SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

UKURASA 4



## Aliyejifungua mguu wa mamba ajisaidia mjusi




UKURASA 9

Jumapili Februari 20, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0580862
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa

# Hatua 6 serikali kudhibiti mauaji

**Polisi,** wabunge, viongozi wa dini, waganga wamulikwa... Uk. 2

*Endelea ukurasa 2*

# TANESCO kuunganishia umeme waliolipa 27,000/-

UKURASA 3



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akitoa heshima za mwisho mbele ya jeneza lililobeba mwili wa Dk. Mwelecele Malecela, aliyekuwa mfanyakazi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) katika viwanja vya Karimjee, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 3

## SAA 24 MABAHARIA ZIWANI MELI IKIZAMA

MABAHARIA 11 wameokolewa wakiwa na hali mbaya kiafya baada ya meli ya MV. Mbayamwezi yenye usajili namba BY 0074 ya Burundi kuzama Ziwa Tanganyika ikitokea Zambia kwenda Burundi Jumatano...

## Dk. Mwinyi aongoza mazishi ya Mwele Dar

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA KAZI KAZI NIGER UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Rais Mwinyi aongoza mazishi ya Dk. Mwele

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameongoza kuaga mwili wa Mkurugenzi wa Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele katika Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Mwele Malecela (58), aliyefariki dunia Alhamis ya wiki iliyopita mjini Geneva, Uswisi.

Dk. Mwele aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Vituo vya Kudhibiti ndani ya shirika hilo, Kanda ya Afrika na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) hadi Desemba 17, 2016.

Mwili wake uliwasili nchini juzi usiku na jana viongozi mbalimbali wa serikali, wastaafu, sekta binafsi na wanasiasa walishiriki kuuaga katika viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam na baadaye ulisafirishwa kwenda Dodoma.

Viongozi wengine walioshiriki kuuaga mwili huo jana ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, Makamu Mwenyekiti Chama Cha Mapinduzi (CCM), Philip Mangula na Naibu Katibu Mkuu wa CCM.

Wengine ni Waziri Mkuu mstaafu, Joseph Warioba, maspika wastaafu; Pius Msekwa na Anne Makinda na mawaziri, wabunge wa Bunge la Tanzania na Afrika Mashiriki na Mkuu wa Majeshi mstaafu, Jenerali Davis Mwamunyange.

Katika salamu zake za rambirambi, Rais Dk. Mwinyi alisema: "Kwa niaba yangu binafsi, kwa niaba ya Mzee Mwinyi na familia ya Mzee Mwinyi, leo wangependa wawapo hapa lakini kwa bahati mbaya wapo nje ya nchi, wanatuma salamu za rambirambi wanamwombea marehemu."

Alisema anamfahamu Dk. Mwele kwa sababu wakati Mzee Malecela na Mzee Mwinyi wanafanya kazi pamoja, familia hizo zilikuwa karibu.

"Nilimfahamu zaidi Mwele katika shughuli za kazi, nikiwa Naibu Waziri wa Afya, Mwele alikuwa akifanya NIMR, akifanya katika nafasi mbalimbali mpaka alipofikia kuwa Mkurugenzi Mkuu, alijitoa na alikuwa mwanataaluma.

"Alipenda kujituma na kutaka mambo yafanikiwe, ameipa sifa NIMR kwa programu alizozianzisha, nikizungumza na washirika wa maendeleo, taasisi za Umoja wa Mataifa, wanamwagia sifa kwa kazi kubwa hususani katika programu za matende na mabusha.

"Ameitumikia nchi yake miaka 30, tunapaswa tujiulize endapo tutaweza kufikia yale aliyofikia Dk. Mwele? Alikuwa mwenye utu mkubwa, alikuwa karibu na watu na alipenda kusaidia. Tujitahidi kuacha hadithi njema kama alivyoiacha Dk. Mwele," alisema.

Akiwasilisha salamu za Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Majaliwa, alisema: "Amenituma nilete salamu hizi kwako (Malecela), watoto, wajukuu kuwa atakapopata nafasi baada ya kurudi nchini, atakuja nyumbani Dodoma kukusalimia."

Majaliwa alisema wamempoteza mtu mzuri ambaye ametoa mchango mkubwa serikalini na kueleza kuwa wana jukumu kubwa la kuenzi yale mazuri aliyofanya ndani na nje ya utumishi wa umma.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia alinukuu kifungu cha Biblia kutoka kitabu cha Wagalatia 6:7 akisema "msidaganyike, apandacho mtu ndicho atakachovuna".

Dk. Tulia aliendelea: "Tulipo hapa tumesikiliza wema wa ndugu yetu aliyelala, ushujaa wa ndugu yetu aliyelala, mchango kwa nchi yake, mchango wake wa kitaaluma, kifamilia na wengine ambao hawahusiki na familia yake."

Salamu za Shule ya Sekondari ya Weruweru, Golden Girls zilitolewa na Dk. Maria Kan, ambaye alisema Mwele aligusa maisha ya wengi na ya mtu mmoja mmoja na alikuwa kiongozi imara na alitumia elimu yake kwa manufaa ya taifa na hakusaliti nchi.

Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Prof. Yunus Mgaya, alisema taasisi hiyo pamoja na Wizara ya Afya watamkumbuka Dk. Mwele kupitia mpango aliouanzisha wa kudhibiti magonjwa ya matende na ngiri maji ambao baadaye serikali iliuhuisha na kuwa wa kitaifa na kuhusisha magonjwa matano.

Spika mstaafu Anne Makinda alisema mambo aliyoyafanya ni makubwa yaliyozidi umri wake na kumwelezea kuwa enzi za uhai wake hakupoteza hata dakika moja, alitenda yanayohusu maisha ya wengine.

Waziri Mkuu mstaafu Warioba alisema: "Mwaka 2015, Mwele alikuja kwangu kutaka ushauri kama achukue fomu kugombea urais, nikamwambia 'Mwele unaona una uzito wa kutosha kuingia katika kundi hili, huoni ugumu?'.

"Alichoniambia 'baba naye amesema hivyo, lakini ninaamini ninaweza'. Aliingia, alijiamini, hakuogopa kitu chochote."

Akizungumza kwa niaba ya chama, Makamu Mwenyekiti wa CCM, Mangula, alimwambia baba wa Dk. Mwele, John Malecela, kuwa chama kipo pamoja naye katika nyakati hizi za majonzi.



Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson, akitoa heshima za mwisho mbele ya jeneza lililobeba mwili wa aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Udhibiti wa Magonjwa ya Kitropiki yasiyopewa kipaumbele wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Dk. Mwelecele Ntuli Malecela katika viwanja vya Karimjee Jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: BUNGE**

# Hatua 6 serikali kudhibiti mauaji

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

WAKATI matukio ya mauaji ya watu yakiendelea kuripotiwa kwenye maeneo mbalimbali nchini, serikali imeagiza hatua sita zichukuliwe kukabiliana na baa hilo.

Katika hotuba yake ya kuahirisha Bunge juzi, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alizitaja hatua hizo bungeni jijini hapa kwamba zinajumuisha kuongeza nguvu ya kiulinzi hadi ngazi ya kata na kuwashirikisha viongozi wa kiroho na kisiasa kukemea uhalifu huo.

Majaliwa aliagiza Jeshi la Polisi nchini liongeze nguvu ya kiulinzi hadi kwenye ngazi ya kata, kufanya oparesheni na misako ya kuwabaini wahalifu wote.

"Fanyeni oparesheni na misako ya kuwabaini wahalifu wote wakiwamo waganga wanaopiga ramli chonganishi na kuchukulia hatua askari, wakaguzi na maofisa wasio waadilifu," aliagiza.

Waziri Mkuu pia aliiagiza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu isimamie utekelezaji wa mipango na mikakati mahsusi ya kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Majaliwa aliwaomba viongozi wa dini waendelee kusaidia suala la malezi ya kiroho ili kujenga jamii yenye ucha Mungu na uadilifu.

"Jeshi la Polisi vilevile lione namna bora ya kushirikisha jamii kupitia ulinzi shirikishi na kutoa taarifa sahihi zitakazosaidia kukabiliana na vitendo vya uhalifu kwenye maeneo yao.

"Nitoe wito kwa waheshimiwa wabunge wenzangu, viongozi wa dini na wadau wote kuunganisha nguvu na kukemea vitendo hivyo, pia hatua kali zichukuliwe kwa wanaojihusisha na vitendo hivyo," aligiza.

**NGORONGORO**

Mbali na baa la mauaji ya watu nchini, Majaliwa alisema serikali ipo tayari kulipa gharama zote kwa wananchi watakaokuwa tayari kuhama kwa hiari ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) ili kulinda hadhi ya eneo hilo.

Alisema wananchi wa Ngorongoro walio tayari kuhamia maeneo mengine kwa hiari yao, wakajiandikishe kwa wakuu wa wilaya za Ngorongoro na Karatu pamoja na Mhifadhi Mkuu na Mkuu wa Mkoa na wapewe ushirikiano unaohitajika.

"Niendelee kusisitiza kuwa wananchi wanaotaka kuhama kwa hiari wasizuiwe na watu wengine wenye lengo la kukwamisha jitahada njema zinazochukuliwa na serikali katika kulinda urithi huu wa dunia na uhifadhi wa maeneo hayo, zoezi litazingatia haki za binadamu," alisisitiza.

Kuhusu kulinda eneo la ushoroba la wanyama Loliondo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,500 ambalo kwa sasa halikaliwi na mtu na halifahamiki vizuri ili kuwezesha jamii na wahifadhi wawe na uelewa wa pamoja, alisema eneo hilo ni muhimu zaidi kwa ajili ya mapito na mazalia ya wanyamapori.

Vilevile, alisema eneo litakalobaki la kilometa za mraba 2,500 wananchi wataendelea na shughuli zao ikiwamo ufugaji.

**FEDHA ZA UVIKO-19**

Alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, kufanya uchunguzi zaidi wa matumizi ya fedha za miradi ikiwamo ya UVIKO-19 na kuchukua hatua stahiki kwa watakaobainika kufanya ubadhirifu.

Majaliwa alisema kuna baadhi ya halmashauri nchini zimebainika kuwa na matumizi yasiyoridhisha ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hususan ya UVIKO-19.

"Kwa msingi huo, ninamwagiza Waziri wa TAMISEMI kufanya uchunguzi zaidi wa matumizi ya fedha za miradi ya UVIKO-19 na miradi mingine ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kinidhamu kwa viongozi na watendaji wote watakaobainika kufanya ubadhirifu,"alisema.

Aliwataka wakuu wa mikoa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa matumizi ya fedha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha inaakisi thamani ya fedha za Watanzania.

"Hata hivyo, kutokana na taarifa za ubadhirifu mkubwa katika baadhi ya Halmashauri serikali itapeleka timu maalum ya uchunguzi ili kujiridhisha na matumizi ya fedha za umma," Majaliwa alihitimisha.

**●Imeandaliwa na Salome Kitomari na Augusta Njoji, DODOMA**

## HABARI KITAIFA

# Hukumu kesi kupinga vileo yakwama tena

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KESI ya Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) dhidi ya Mwanasheria Mkuu na Bodi ya Udhibiti Vileo (ZLB) imekwama kutolewa hukumu ndogo kwa mara ya tatu na Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar, Abdulhakim Issa Ameir.

Jaji Abdulhakim alisema juzi kuwa hukumu dhidi ya pingamizi zilizowasilishwa na Mwanasheria Mkuu kupitia wanasheria wa serikali, bado haijakamilika kuandikwa.

Alisema hukumu ya kesi hiyo sasa itatolewa Febuari 28 mwaka huu baada ya kukamilika kuandikwa na kufanyiwa mapitio ili kutoa msimamo wa kesi ya msingi ambayo imefunguliwa na JUMAZA.

"Hukumu ilikuwa itolewe leo (jana) lakini bado haijakamilika kuandikwa, tumeaihirisha kesi," alisema Jaji Abdulhakim.

Wakili anayewakilisha JUMAZA katika kesi hiyo, Ruhaia Kassim Mgeni, alidai wamekubali uamuzi wa jaji kuaihirisha kwa mara ya tatu kutoa hukumu ya kesi hiyo mpaka Febuari 28 mwaka huu.

"Hukumu ya kesi ya JUMAZA dhidi ya Mwanasheria Mkuu na Bodi ya Udhibiti Vileo imekwama kutolewa kwa sababu jaji bado hajakamilisha kufanya mapitio ya hukumu yake," alidai Mwanasheria Ruhaia.

Katika pingamizi zilizowasilishwa na Mwansheria Mkuu wa Zanzibar kupitia wanasheria wa serikali wanadai JUMAZA, imefungua keasi dhidi ya serikali kinyume cha sheria bila ya kutoa taarifa ndani ya siku 60 ya kushtaki serikali kabla ya kufungua kesi wakati ni kinyume cha sheria.

JUMAZA katika kesi ya msingi wanadai Mwanasheria Mkuu na Bodi ya Udhibiti Vileo wamevunja Sheria ya Udhibiti wa Vileo ya Mwaka 2020 baada ya kutoa vibali kwa kampuni zaidi ya tatu kuingiza vileo Zanzibar.

Kesi hiyo imeibua mjadala mkubwa kwa viongozi wa dini, vyama vya siasa na wanaharakati baada ya sheria hiyo kukwama kufanya kazi tangu kupitishwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na kutiwa saini na aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, Mei 11, 2020.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Sophia Mjema, akizungumza mara baada ya kusikiliza kero za wananchi katika kijiji cha Ipeja wilayani Kishapu na kuzitafutia ufumbuzi, zikiwamo ukosefu wa huduma ya umeme, maji, zahanati, na ubovu wa miundombinu ya barabara, jana.**PICHA: MARCO MADUHU**

# TANESCO kuunganishia umeme waliolipa 27,000/-

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) limezindua rasmi mkakati wa kuhakikisha linawaunganishia nishati ya umeme wateja wake wote waliolipia Sh. 27,000 ambao kwa nchi zima ni zaidi ya 90,000.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Msemaji wa TANESCO, Martin Mwambene, alisema huo ni mkakati ambao unafanyika nchi zima, akibainisha kuwa kwa Dar es Salaam wameanzia mkoa wao wa Temeke utakaofuatiwa na Kigamboni na Mikwembe.

"Oparesheni hii itafanyika katika mikoa yote ya ki-TANESCO nchini tukiwa na lengo la kuhakikisha tunamalizana na wateja wote na tunachotaka sasa hivi ni mteja anayelipia leo basi ndani ya siku mbili au tatu apate kuunganishiwa tofauti na ilivyokuwa huko nyuma," alisema. Meneja wa TANESCO Mkoa wa Temeke, Sotco Nombo, alisema kuwa katika eneo hilo watahakikisha ifikapo mwishoni mwa mwezi ujao wateja waliolipia Sh. 27,000 wawe wameunganishiwa angalau kwa asilimia 95.

Alibainisha kuwa hadi jana, idadi ya wateja waliolipia kiwango hicho mkoani ilikuwa 8,955.

Aliongeza kuwa kwa siku wamejiwekea utaratibu wa kuunga wateja kati ya 250 hadi 300 na kazi inafanyika hadi siku za mapumziko.

"Tunavyounga kwa sasa tunaenda kimaeneo lakini mpango wetu hata wale ambao wamelipia hivi karibuni tutakavyokuwa tunaendelea na mpango huu hatutachagua kwamba huyu kalipia lini, tutawafungia wote na hii ni ili kupunguza gharama kwamba tusiwe tunakwenda sehemu moja halafu kesho tukarudi," alisema Nombo.

Alibainisha kwamba ili kuboresha huduma zao wameanzisha utaratibu wa kukusanya taarifa za wateja wao ili kuziingiza katika mfumo wao wa GIS ili mteja anapopata tatizo wamfikie kwa wakati.

Aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano wa kutosha na endapo watapata kikwazo wawasiliane nao kwa namba 0748 550 000 ili wapatiwe ufafanuzi.

Baadhi ya wananchi walionufaika na huduma hiyo, akiwamo Salimu Ramadhani, mkazi wa Kijichi, waliipongeza TANESCO kwa hatua hiyo, wakisisitiza imewasaidia kuwatoa katika adha ya giza ambayo imekuwa ikiwakabili kwa kipindi kirefu.

"TANESCO iendelee na kasi hii kwani kitendo cha kutufungia umeme kimesaidia kuchochea zaidi biashara zetu, mwanzo tulikuwa tunashindwa kuuza vinywaji kutokana na matakwa ya wateja wengi wanataka vya baridi, hivyo tunapongeza sana shirika kwa kuhakikisha wanatusogezea huduma hii," alipongeza Ramadhani.

Aisha Iddy, mkazi wa Mbagala, alisema uamuzi huo wa TANESCO utawasaidia hata katika kuboresha ulinzi, akifafanua kuwa awali ikifika majira saa moja usiku, walikuwa wanafunga biashara zao lakini kwa sasa hawatakuwa na haraka ya kufunga kutokana na umeme kuwapo, hivyo kuangaza vyema mazingira yao.

# Saa 24 mabaharia ziwani meli ikizama

**Na Ibrahim Yassin,** RUKWA

MABAHARIA 11 wameokolewa wakiwa na hali mbaya kiafya baada ya meli ya MV. Mbayamwezi yenye usajili namba BY 0074 ya Burundi kuzama Ziwa Tanganyika ikitokea Zambia kwenda Burundi Jumatano.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Willium Mwampagale, alisema meli hiyo ni mali ya Rafiki Ibrahimu chini ya Kampuni ya Red Marine ya Burundi.

Alisema ilizama Ziwa Tanganyika kwenye maeneo ya Kabwe wilayani Nkasi mkoani Rukwa baada ya kupigwa na dhoruba kali Februari 17 majira ya saa tano asubuhi.

Alibainisha kuwa meli hiyo ilitoka Mpulungu, Zambia kwenda Burundi Jumanne ya wiki hii ikiwa imebeba malighafi ya kutengenezea saruji ikiwa chini ya usimamizi wa mabaharia 11 ambao sita ni raia wa Kongo, watano raia wa Burundi na Mtanzania mmoja.

"Siku iliyofuata (Februari 17 mwaka huu), walipofika eneo la Kabwe wilayani Nkasi, walikumbana na dhoruba kali iliyopelekea meli hiyo kuyumba na kuzama," alisimulia.

Kamanda Mwampaghale alidai kuwa baada ya meli hiyo kuzama, mabaharia hao walivaa vifaa vya kujiokoa na walikaa majini saa 24 hadi walipookolewa na askari kutoka Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi (JWTZ) waliofuatana na wavuvi.

Alisema jitihada za kuwaokoa mabaharia hao zilizaa matunda na kwamba baada ya kuokolewa, walipelekwa katika Kituo cha Afya Kirando kwa ajili ya matibabu.

"Wakati wanaokolewa walikuwa katika hali mbaya, kwenye kituo cha afya walipata huduma ya kwanza na kupata nafuu na hadi sasa wanaendelea vizuri," alisema.

Nahodha wa meli hiyo, Ramadhan Katambo, alidai kuwa baada ya meli hiyo kuzama, alikuwa wa kwanza kutoka ndani ya meli hiyo na kupiga mbizi huku akipiga mayowe kuomba msaada ndipo wavuvi walipojitokeza kwenda kutoa msaada wa kumwokoa na kuwaokoa wengine.

Alisema kuwa meli hiyo yenye uwezo wa kubeba tani 18, siku hiyo ilibeba mzigo wa tani 17, akisisitiza kuwa uzito ulikuwa sahihi, lakini ajali ilisababishwa na upepo mkali.


Victoria FINANCE

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

**VICTORIA FINANCE PLC** INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MICHAEL SAMUEL KYANDE AS LEGAL ADMISTRATOR OF THE ESTATES OF THE LATE FILLY NDEONANSIO | NYUMBA | HATI YA NYUMBA – TABATA MWANANCHI | KISAONI AUCTION MART TANZANIA LTD | 07-03-2022 |
| 2 | ALLAN ABEL MUSHI T/A GETRUDE KAVISHE | PAGALE | LESENI YA MAKAZI – TEMEKE YOMBO | DIAMOND RECOVERIES | 07-03-2022 |
| 3 | SELINA SEVERINI MTENGA AS LEGAL ADMISTRATOR OF THE LATE GODLIVING O. MANGOWI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – MLANDIZI PWANI | ACCURATE RECOVERY LTD | 07-03-2022 |
| 4 | RAJABU HAMIS BADI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KIMARA | ACCURATE RECOVERY LTD | 07-03-2022 |
| 5 | HASSAN JUMA MRISHO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - DAKAWA | HOLLYNESS AND RESPISHERS CO LTD | 07-03-2022 |
| 6 | ABDALLAH HAMIS GOBETO | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI - DAKAWA | HOLLYNESS AND RESPISHERS CO LTD | 07-03-2022 |
| 7 | DOREEN MCHAWA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - KINYEREZI | AMA'Z | 07-03-2022 |
| 8 | SWEDY HAMIS SWEDY | NYUMBA | HATI YA NYUMBA – KIGOGO FRESH PUGU | ACCURATE RECOVERY LTD | 07-03-2022 |
| 9 | SALIMU MWAKING'INDA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - UNUNIO | ACCURATE RECOVERY LTD | 07-03-2022 |
| 10 | FELIX KIMARO. DAUDI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO-N UBUNGO | KISAONI AUCTION MART TANZANIA LTD | 07-03-2022 |
| 11 | CYPRIAN KIHALALWA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MKUNYWA MADIBIRA | HOLLYNESS & RESPISHERS LTD | 07-03-2022 |
| 12 | ROJAS MPULULE | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA | HOLLYNESS & RESPISHERS LTD | 07-03-2022 |
| 13 | ERASTO MNDEME | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA | HOLLYNESS & RESPISHERS LTD | 07-03-2022 |
| 14 | IBRAHIM MNDEME | PAGALE | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA | HOLLYNESS & RESPISHERS LTD | 07-03-2022 |
| 15 | KALIMEL LIHO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA | HOLLYNESS & RESPISHERS LTD | 07-03-2022 |
| 16 | FATNA NZOWA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA | HOLLYNESS & RESPISHERS LTD | 07-03-2022 |
| 17 | ZENA NYON | KIWANJA | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA | HOLLYNESS & RESPISHERS LTD | 07-03-2022 |
| 18 | JUMA NYAKASONGA | PAGALE | MKATABA WA MAUZIANO- MAHANGO MADIBIRA | HOLLYNESS & RESPISHERS LTD | 07-03-2022 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

# Aliyejifungua mguu wa mamba ajisaidia mjusi

**Na Ibrahim Yassin,** KYELA

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, Maria Mwakila (26), mkazi wa Kitongoji cha Mbyaso, Kijiji cha Mpunguti, Kata ya Ikama wilayani Kyela mkoani Mbeya, amejikuta katika wakati mgumu baada ya kutokwa na mjusi sehemu za siri alipokwenda kujisadia haja ndogo.

Wiki tatu zilizopita, kijana huyo aliripotiwa kujifungua mkono wa mamba na kuzua taharuki kwa wakazi wa eneo hilo.

Ilidaiwa kuwa kijana huyo alikuwa na ujauzito wa miezi mitatu na alitibiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela baada ya kukumbana na mkasa huo.

Siku 18 baada ya kupata matibabu hayo, jana majira ya saa mbili asubuhi, alipokwenda kujisaidia haja ndogo, alidai ulitoka mjusi ukiwa na kucha mkiani.

Akizungumza jana na Nipashe Jumapili baada ya kumaliza kikao cha machifu, mume wake, Lugano Sindalama, alisema walioana Oktoba mwaka jana baada ya kuwa ameachana na mwanamume aliyekuwa naye wilayani Sumbawanga.

Mume wake huyo alidai kuwa baada ya kupata ujauzito, mke wake alikumbana na matatizo mengi ikiwamo kuugua mara kwa mara.

Alisema kuwa ilipotimu miezi mitatu ya ujauzito huo, alianza kujisikia dalili za uchungu na walipomwahisha hospitalini alipona na kurejea nyumbani lakini siku hiyo hiyo aliyotoka hospitalini, akiwa sebuleni, alijisikia kama ameshikwa na haja ndogo, alipofika eneo la kujisitiri, alijikuta akitokwa na mkono wa mamba huku damu nyingi ikimtoka.

Aliongeza kuwa baada ya tukio hilo ilibidi akimbizwe hospitalini na kupatiwa matibabu ikiwa ni pamoja na kusafishwa tumbo ambapo waliondoa uchafu uliokuwamo na baada ya wiki tatu akiwa katika hali safi na salama akajikuta anajisaidia mjusi ulio na mkia wenye kucha.

Alisema baada ya hapo wazee wa kimila waliitisha kikao cha machifu na familia zao kujadili sintofahamu hiyo na namna ya kuidhibiti.

Atupakisye Mwamakula, Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, alisema ni tukio la kwanza kutokea katika eneo lao na pia waliposikia mwanamke amejifungua mkono wa mamba waliona ni jambo la kawaida kwa kuwa maeneo mengi huwa yanatokea.

Alisema kuwa tukio la pili walipolisikia amejisaidia mjusi, walishikwa na butwaa ndipo walipoitisha kikao ili wajue tatizo na kulitafutia ufumbuzi.

Akizungumzia hali hiyo, Maria alisema anamwachia Mungu, akiamini ipo siku atajifungua mtoto wa kawaida asiyekuwa na dosari.

Chifu Mkuu wa Kijiji hicho, Magojanya Mwaluswa, alisema wamekemea kitendo hicho na kushauri familia zinazovutana na kuwa kile wanachoamini ni kiini cha tatizo, zimalizane kwa kuwa kijiji hicho na vitongoji vyake havina historia ya matukio hayo.



Mke wa Rais wa Zanzibar ambae pia ni Mwenyekiti wa Zanzibar Maisha Bora Foundation, Mama Mariam Mwinyi (watatu kulia mstari wa mbele) akiwasalimia Wananchi katika mitaa ya Michenzani wakati wa Matembezi ya Uzinduzi wa Taasisi yake ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (kulia kwake) Mke wa Rais Mstaafu, Mama Salma Kikwete, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Mhandisi Zena Ahmed Said na kushoto kwake Mke wa Waziri Mkuu Mama Mary Majaliwa wakiwa katika matembezi hayo, yaliyoanzia Kiembesamaki na kumalizia katika viwanja vya Mao Zedung. **PICHA: IKULU.**

# Taasisi sita zaingia ubia kutafuta gesi na mafuta

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuendeleza juhudi za utafutaji na upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi asilia, taasisi sita za Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Tanzania zimesaini hati za makubaliano ya ushirikiano katika rasilimali hizo.

Utiaji saini huo umehusisha Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta Zanzibar (ZPRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (EWURA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA).

Taasisi zingine ni Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC), hafla ikifanyika jana kwenye Hoteli ya Verde mjini Zanzibar.

Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, alisema ushirikiano kati ya taasisi za Muungano katika masuala ya utafiti wa nishati na gesi ni muhimu kwa ajili ya kujenga nguvu na uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa pamoja.

Mramba alisema Tanzania Bara imeanza muda mrefu kufanya utafiti wa nishati ya mafuta na gesi ambapo tayari uzalishaji wa gesi umeanza zaidi ya miaka sita sasa kwa mafanikio makubwa.

Alibainisha kuwa mpaka sasa zaidi ya futi za ujazo trilioni 57 za gesi asilia tayari zimegundulika.

Akifafanua zaidi, kiongozi huyo alisema ushirikiano huo ni muhimu kufanyika kwa pamoja na wenzao wa Zanzibar ambao wako katika mchakato wa kazi za utafutaji wa mafuta na gesi kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

"Tumefungua ushirikiano wa pamoja wa nishati ya mafuta na gesi pamoja na utafiti wake ili kuona tunakwenda pamoja, hatua ambayo itaongeza ufanisi," alisema.

Aliongeza kuwa ushirikiano huo utasaidia katika kubadilisha utafiti na mbinu pamoja na utaalamu kwa wafanyakazi wa pande mbili za Muungano.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Mgereza Miraji Mzee, alisema ushirikiano huo umelenga kuimarisha Muungano katika sekta muhimu ya kimkakati ya mafuta na gesi.

Alisema Serikali ya Zanzibar iko katika utafiti wa rasilimali ya mafuta na gesi katika hatua mbalimbali ambapo ushirikiano huo sasa unafunguwa milango ya mategemeo katika kupata wataalamu wenye uwezo wa kazi hizo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Petroli nchini, Dk. James Mataragio, alisema wako tayari kufanya kazi na kutoa uzoefu wa kitaalamu kwa upande wa Serikali ya Zanzibar ambayo iko katika mchakato wa utafiti na utafutaji wa nishati ya mafuta na gesi.

"Makubaliano ya utiaji saini wa taasisi sita zinazofanya kazi na kutoa huduma masuala ya nishati na gesi ni muhimu ambapo kwa upande wetu TPDC tupo tayari kufanya kazi na kubadilisha uzoefu na wenzetu kutoka Zanzibar katika safari ya kutafuta mafuta na gesi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mjini Unguja, Rashid Simai Msaraka, alisema utiaji saini wa taasisi hizo ni kiashiria kikubwa cha Muungano ulioasisiwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na kuifanya Tanzania kuwa na nguvu kuliko nchi zingine katika Bara la Afrika.

## JK aipongeza AGRA kuwafikia wakulima

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

RAIS mstaafu wa awamu ya nne na Mjumbe wa Bodi wa Shirika la Mapinduzi ya Kijani Barani Afrika (AGRA), Dk. Jakaya Kikwete, amelipongeza shirika hilo kwa kuwafikia wakulima milioni 1.5 nchini kwa kuwapa maarifa ya kilimo.

Mbali na pongezi hiyo, kiongozi huyo pia amesema shirika hilo limefanikiwa kutoa mafunzo kwa wanasayansi 41 katika ngazi tofauti ambao wanasaidia kuwapa elimu wakulima wadogo nchini.

Akizungumza jijini Dodoma jana wakati akizindua kitabu cha kuongeza ushindani wa biashara za kilimo na mifumo yake kwa wakulima wadogo, Dk. Kikwete alisema shabaha kubwa ya AGRA ni kuleta mageuzi katika kilimo ambayo yanaleta tija kwa wakulima wadogo nchini.

Alisema ukizungumzia mageuzi ya kilimo Afrika, sehemu kubwa iko mikononi mwa wakulima wadogo, hivyo ukitaka kuleta mageuzi ya kilimo ambayo ni jumuishi, hupaswi kulisahau kundi hilo kwa sababu ni muhimu katika sekta ya kilimo.

"Katika kufanya mageuzi ya kilimo ukishawasahau wakulima wadogo, mageuzi hayo yatakuwa yamewaacha watu wengi sana kwenye kilimo. Ndio maana AGRA inalenga zaidi kwa wakulima wadogo," alisema.

Dk. Kikwete alisema AGRA katika kufanya shughuli zake, inafanya kazi na serikali katika maeneo ambayo inataka wasaidie na mara nyingi wanafanya msaada wa kuwajengea uwezo wakulima katika masuala ya sera na kuboresha mifumo ya kilimo nchini.

Alisema moja ya mambo ambayo taasisi hiyo inayaangalia ni uzalishaji mbegu ambapo wamesaidia kutoa elimu kwa wakulima ambao hivi sasa wanalima ekari moja huku wakipanda mbegu bora wanapata magunia 25 hadi 30 tofauti na awali walikuwa wakipata magunia matatu.

"Nawapongeza sana AGRA kwa sababu wameonyesha nini maana ya shabaha ya mageuzi katika kilimo," alisifu.

Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, alisema kuwa katika ziara ya siku tano wameweza kujifunza mambo mengi kutoka kwa Rais mstaafu Kikwete ikiwamo kupata elimu kwenye kilimo.

Alisema kazi kubwa aliyoifanya Dk. Kikwete ni kuifanya AGRA ijulikane zaidi kutokana na ujumbe wa masuala ya kilimo ambao imetoa kwa wakulima.

# Kampuni yakabidhi madarasa mapya

**Na Mwandishi Wetu,** SENGEREMA

KAMPUNI ya OreCorp Tanzania Limited imeendela kuiunga mkono Wilaya ya Sengerema kwa kukamilisha na kukabidhi madarasa matatu mapya ya Shule ya Sekondari ya Ngoma kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa OreCorp, Matthew Yates na Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa OreCorp, Henk Diederichs, ambao walihudhuria hafla ya makabidhiano hayo juzi wakitokea makao makuu ya kampuni hiyo Australia, kukabidhiwa kwa madarasa hayo ni hatua kubwa ya ushirikiano baina ya pande hizo.

Walibainisha kuwa kampuni hiyo ilipewa leseni maalumu ya uchimbaji Desemba 13, 2021 kupitia Kampuni ya Sotta Mining Corporation Limited (SMCL) ambayo inaundwa kwa ushirikiano baina ya serikali ya Tanzania (asilimia 16) na OreCorp (asilimia 84), kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa Mgodi wa Dhahabu wa Nyanzaga kusini mwa Kata ya Ngoma wilayani Sengerema.

Meneja Mkuu wa OreCorp Tanzania, Damien Valente, alisema: "OreCorp inafurahia mchango wake endelevu wa kuwapatia watoto mazingira bora na salama yanayowawezesha kujifunza na kuendelea na masomo yao."

Ujenzi wa madarasa hayo ni sehemu ya miradi ya uwezeshaji jamii ya hivi karibuni ambayo OreCorp imekamilisha tangu ianze kuendesha mradi huo mwaka 2015.

Julai mwaka jana, OreCorp ilitoa Sh. milioni 26 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo na madawati kwa ajili ya Shule ya Sekondari Ngoma na kampuni hiyo imekuwa ikitekeleza mipango kadhaa ya uwezeshaji jamii wilayani humo ikiwamo kutoa Sh. milioni 45 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo kipya cha Polisi Ngoma Aprili mwaka jana.

Ujenzi wa madarasa hayo mapya uliidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya Desemba 8, 2021 na ulianza rasmi Januari 11, mwaka huu.

Madarasa haya yamedhaminiwa na OreCorp kama sehemu ya mpango wake wa kuiwezesha jamii kwa kuzingatia mpango wa kuiendeleza jamii ulioidhinishwa.



Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Macho, Catherine Makuba (kushoto), akimpima macho mkazi wa Kibaha mkoani Pwani, Joyce Mbuli, wakati wa uzinduzi wa kambi ya siku tano iliyoandaliwa na Taasisi ya Qatar Charity ya Qatar iliyojitolea kutoa huduma hiyo bure kwa wananchi wa Kibaha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Mfumo mpya upimaji wa watumishi waiva

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imekuja na mfumo mpya wa kupima utendaji kazi wa watumishi wa umma (OPRAS) utakaopima utendaji wa kila siku wa mfanyakazi ikiwamo matokeo ya utendaji kazi wa kila taasisi unaotarajiwa kuanza Julai Mosi mwaka huu.

Akizungumza juzi jijini hapa na watumishi wa Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alisema mfumo huo mpya ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, akisisitiza utasaidia kwa kiasi kikubwa kuonyesha taasisi zinazofanya kazi kwa bidii na zinazolegalega.

Alisema Sekretarieti ya Ajira inapaswa kuwa mfano katika utendaji kazi mzuri kwa kuwa wao ndio wanaoendesha hiyo mifumo lakini pia ni watumishi wa umma.

"Ninyi mnapaswa kuwa mfano mzuri kwa watumishi wa taasisi zingine kwa sababu lengo ni kuangalia utendaji kazi. Kwa hiyo, mifumo hii ianze kuonyesha utendaji kazi wenu mzuri ili na wengine waige kutoka kwenu," aliagiza.

Pamoja na hilo, alisema serikali imeanzisha mifumo mingine ya TEHAMA ikiwamo mfumo wa mrejesho unaomwezesha mwananchi kutoa maoni yake kuhusiana na utendaji kazi wa utumishi wa umma.

Kuhusu suala la rushwa, waziri huyo alisema Tanzania imefanya vizuri kutokana na kuzingatia misingi ya utawala bora ambapo kati ya nchi 180 duniani, Tanzania imeshika nafasi ya 87, huku ikishika nafasi ya pili Afrika Mashariki ikitanguliwa na Rwanda.

Aliwataka watumishi hao kuzingatia matumizi ya lugha nzuri wakati wa kutoa huduma kwa wateja ili kueleza shida zao pale wanapohitaji huduma kutoka taasisi hiyo.

Kaimu Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira, Samwel Tanguye, alisema moja ya kero wanazokumbana nazo ni

# Rais Samia kuzuru mkoa wa Pwani

**Na Waandishi Wetu,** KIBAHA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kufanya ziara ya kichama ya siku moja na kufungua Chuo cha Uongozi wa Siasa cha Mwalimu Nyerere kilichojengwa kwa ushirikiano wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na vyama vilivyoshiriki ukombozi wa Bara la Afrika Kwamfipa, Kibaha mkoani Pwani.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa jana, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliwataka wakazi wa mkoa huo kujitokeza kwa wingi kumpokea Rais na viongozi wengine kutoka nje ya nchi.

Kunenge alisema katika hafla hiyo ya uzinduzi huo, viongozi wa vyama vya siasa kutoka kwa vyama vilivyoshiriki ujenzi wa chuo hicho, wanatarajiwa kushiriki.

Alisema kuwa kwa mujibu wa taarifa za chama, kabla ya ziara ya Rais Samia, Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, anatarajiwa kuzindua barabara iliyojengwa kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita mbili ambayo inaelekea katika chuo hicho.

Kunenge alisema kuwa katika uzinduzi wa barabara hiyo, Chongolo atafuatana na makatibu wakuu wengine wa vyama vya siasa vilivyojenga chuo hicho.

Chuo hicho kinahusisha vyama sita vya ukombozi barani Afrika ambavyo ni: CCM (Tanzania); FRELIMO (Msumbiji); ANC (Afrika Kusini); SWAPO (Namibia); ZANU-PF na MPLA (Zimbabwe).

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Shule ya Sekondari Zogowale iliyoko Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Tatu Mwambala ameishukuru serikali kwa kuidhinisha Sh. milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na ununuzi wa madawati zaidi ya 100.

Tatu alisema jana shuleni huko kuwa miundombinu hiyo imeongeza ari na moyo wa kujifunza na kufundisha kwa kuwa sasa wanafunzi wanakaa vizuri kwenye madarasa yaliyojengwa kisasa.

Salma Shomari na Subira Amosi wanaosoma kidato cha tano shuleni huko, waliishukuru serikali kwa ujenzi huo, wakitamba kuwa sasa wanao uhakika wa kupata ufaulu wa juu.

Halmashauri ya Mji Kibaha ilipata Sh. milioni 940 ambazo zimejenga madarasa 47 kwenye shule za sekondari na kununua madawati zaidi ya 1,300 kutoka mgawo wa fedha za tozo za miamala ya simu na mkopo wa kukabiliana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19.

• **Imeandikwa na Yasmine Protace na Julieth Mkireri**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hoja kuundwa chombo huru kuchunguza polisi ni muhimu

**WIKI** hii, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kiliandaa semina kwa wabunge kuhusu masuala ya utetezi wa binadamu mjini Dodoma huku wawakilishi hao wa wananchi wakitoa mapendekezo yanayolenga kuleta utawala bora unaozingatia sheria nchini.

Kubwa katika mambo ambayo yalitolewa na wabunge 20 wanaojipambanua kama vinara wa kutetea haki za binadamu ni kufumuliwa kwa muundo wa Jeshi la Polisi na kuundwa kwa chombo huru ambacho pamoja na mambo mengine, kitachunguza nidhamu ya askari polisi pamoja na matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu dhidi ya raia.

Wabunge hao, katika mapendekezo yao, walisema kuna mambo mengi ndani ya Jeshi la Polisi ambayo yanalazimu kufumua muundo mzima ili kutoa baadhi ya vitengo na kuondoa au kupunguza malalamiko ya vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu.

Sambamba na kufumuliwa na kuwapo kwa vitengo vinavyojitegemea, walisema hatua hiyo itawezesha jeshi hilo lenye dhamana ya usalama wa raia na mali zao, kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuendana na karne ya 21 ya sayansi na teknolojia. Walibainisha kuwa pamoja na mabadiliko ya teknolojia, polisi bado wamebaki na mbinu zile zile, maarifa yale yale katika utendaji kazi, ndiyo maana matukio ya watu kutendwa ubaya yanaongezeka.

Katika kujenga hoja yao, wabunge hao walionyesha kuwa wamefanya utafiti wa kutosha kwa kubainisha kuwa katika baadhi ya nchi kuna vitengo vimeshatenganishwa kama vile vitengo vya upelelezi na uendesha mashtaka tofauti na sasa ambapo katika baadhi ya kesi polisi wanapeleleza na kuendesha zinapofikishwa mahakamani. Kwa hatua hiyo, inaonekana haki haiwezi kutendeka kwa taasisi moja kuchunguza na kusimamia kesi.

Miongoni mwa mifano waliyoitolea ni Zanzibar baada ya kuundwa kwa chombo huru ndani ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na kuwekwa katika Katiba, hivyo wananchi kuwa na uhuru kwenda kutoa taarifa pindi wanaponyanyaswa au kutendewa vitendo viovu na polisi kinyume cha sheria.

Wazo la kuwapo kwa chombo au taasisi huru itakayotambulika kisheria na kuwekwa katika Katiba kama ilivyopendekezwa na wabunge hao, limetolewa kwa wakati mwafaka kutokana na hali halisi inayoendelea sasa kuhusu tuhuma za polisi za ukiukwaji wa haki za binadamu. Hivi karibuni mathalan, polisi walidaiwa kumwua mfanyabiashara wa madini mkoani Mtwara na wakati jambo hilo likiwa bado moto, polisi wenyewe, ambao ndio walalamikiwa wakuu, walianza kuchunguza suala hilo hadi Rais Samia Suluhu Hassan alipoingilia kati ka kuagiza iundwe tume kuchunguza madai hayo.


Ni dhahiri kwamba katika utawala wa sheria, mtumishi au kikundi cha watu ndani ya taasisi wanaotuhumiwa kufanya jambo kinyume cha kanuni na taratibu ikiwamo kukiuka haki za binadamu kama vile kutesa au kuua watu, haiwezekani wakajichunguza. Kwa asilimia kubwa ukweli utafichwa kwa sababu ya kulindana.

Kuna umuhimu wa kuundwa kwa taasisi au chombo huru kuchunguza mienendo pamoja na vitendo vinavyofanywa na askari polisi kwa sababu kwa sasa sifa ya jeshi hilo imeporomoka kiasi cha kuwafanya wananchi kukosa imani nalo.

Vitendo vya mahabusu kupoteza maisha kwa madai ya vipigo wakiwa rumande, wananchi kukamatwa na kuporwa mali zao na polisi, baadhi ya askari kutuhumiwa kushiriki matukio ya ujambazi na kuwalinda wahusika wa vitendo hivyo na kukithiri kwa rushwa ndani ya jeshi hilo, ni ushahidi tosha wa kupoteza sifa na wananchi kukosa imani.

Kutokana na tuhuma hizo, ndiyo maana hata Rais Samia mara kadhaa aliagiza uongozi wa jeshi hilo kujitafakari na kuchukua hatua. Kwa mantiki hiyo, ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na imani tena na haki kutendeka, chombo huru cha kuchunguza vitendo vya askari polisi ni lazima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Huku nako kuna kero, viongozi TANESCO waimulike

**WIKI** hii, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) ilisema imebaini kwamba taasisi nyingi za umma zinafanya kazi kama ziko katika nchi mbili zenye mirengo tofauti.

Miongoni mwa taasisi hizo ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambalo kamati hiyo ilisema imeshindwa kuunganisha umeme katika mgodi wa dhahabu wa Biharamulo unaosimamiwa na kampuni ya STAMIGOLD inayomilikiwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

Hali hiyo imebainika na kamati imeona taasisi nyingi za umma hazifanyi kazi kwa kushirikiana licha ya dhamira ya taasisi zote kuwa ni kujenga uchumi imara wa Tanzania.

Hayo yamo katika taarifa ya kamati hiyo iliyowasilishwa bungeni jijini Dodoma na Mwenyekiti wake, Jerry Silaa, na kusema bunge linaitaka serikali kuhakikisha kila taasisi inatekeleza wajibu wake kwa wakati na kwa ufanisi ili kurahisisha utekelezaji wa miradi na majukumu ya taasisi nyingine.

Nimejaribu kueleza kwa kifupi kile ambacho kilijiri bungeni kuhusu kero hiyo ya kushindwa kuunganisha umeme katika mgodi wa dhahabu lakini ninataka kujadili kero kama hiyo kwa ngazi ya chini.

Miaka michache iliyopita, ilikuwa rahisi mtu kulipia huduma ya umeme na kuunganishiwa nyumbani haraka bila kuchelewa. Pia mteja anapokuwa na tatizo, akitoa taarifa tu, wafanyakazi shirika hilo wanakuja haraka.

> **Miaka michache iliyopita, ilikuwa rahisi mtu kulipia huduma ya umeme na kuunganishiwa nyumbani haraka bila kuchelewa. Pia mteja anapokuwa na tatizo, akitoa taarifa tu, wafanyakazi shirika hilo wanakuja haraka.**

Lakini sasa ni kama kasi ya utendaji huo imepungua kwani mteja anaweza kulipia umeme lakini wafanyakazi wasije kumwunganishia kwa wakati na zaidi ya hapo ni kauli kwamba 'subiri utaunganishiwa'.

Miaka ya nyuma mtu akihitaji kuunganishiwa umeme katika nyumba yake, akishalipia, ilikuwa inachukua mwezi mmoja au chini ya hapo hali iliyowafanya wateja kuchangamka kuunganishiwa umeme.

Katika mazingira hayo ya kusubiri kuunganishiwa umeme, wako baadhi ya wateja wanaodai kwamba walilipia huduma hiyo Septemba, mwaka jana, lakini hadi sasa hawajapata huduma.

Iwapo aliyeomba kuunganishiwa umeme anahitaji kufanya biashara ya juisi na vitu vingine vidogo kwa ajili ya kuhudumia familia yake na kujiongezea kipato, ni wazi kwamba atakuwa amekwama kutokana na kukosa huduma hiyo kwa wakati.

Huduma hizo hafifu zimekuwa zikilalamikiwa na wananchi kutoka maeneo mbalimbali nchini kwamba zinaweza kuwa zinachangia kurudisha nyuma kimaendeleo kutokana na kuchukua muda mrefu kushughulikia kero zao.

Kero nyingine ambayo huwa inatajwa na wananchi ni pale mvua inaponyesha tu umeme unakatwa na kuchukua muda mrefu kurejeshwa na kwamba hata ukirejeshwa, wakati mwingine unaweza ukawa unakatika na kuwaka.

Hali hiyo inaweza kusababisha vifaa vyao vinavyotumia nishati hiyo kuharibika na wamekuwa wakitamani shirika hilo kuwa na mfumo wa utoaji wa huduma hiyo, ambao si kero kwao.

Lakini pia kero nyingine ambayo hulalamikiwa ni pale wafanyakazi wa shirika hilo wanapokosea na kupitisha nyaya za umeme kwenye kiwanja cha mtu na kwamba wanapoombwa kuziondoa wakati mwingine hawafanyi hivyo.

Malalamiko hayo na mengine mengi kuhusu utendaji wa baadhi ya watumishi wa shirika hilo, ni vyema yangepatiwa ufumbuzi wa kudumu ili wateja wahudumiwe kwa wakati.

Kwa mfano, yanapojitokeza makosa kama hayo ya wafanyakazi kupitisha nyaya za umeme kwenye viwanja vya watu na kuombwa waziondoe, ni vyema wakaziondoa ili kutoleta sintofahamu kati yao na wenye viwanja.

KWA MASLAHI YA TAIFA

# Upendo wa kweli ni kuonyesha, si kuonyeshea



Na Pascal Mayalla

JUMATATU ya wiki iliyopita, yaani Februari 14, Watanzania walijiunga na watu wa mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Wapendanao, maarufu kama Valentine Day. Ni siku ambayo huadhimishwa kwa watu kuonyeshana upendo na kupeana zawadi mbalimbali. Hii ni kuonyesha upendo, wakiwemo wapenzi kupeana maua na zawadi.

Kabla sijazama ndani kuzungumzia upendo wa siku hii ya Valentine, naomba kuchukua fursa hii, kuipongeza Kampuni ya mafuta ya TotalEnergies Tanzania, kwa kipindi cha miaka kadhaa mfululizo, kwa kuadhimisha siku hii kwa konyesha upendo wa kweli kwa kuwapa zawadi mbalimbali Watanzania, badala ya kuonyeshea. Kwa kampuni hiyo, maadhimisho hayo si ya siku moja kama Valentine inavyoadhimishwa Februari 14 tu, bali huadhimisha kwa siku 14 mfulululizo.

Kwa mazoea yalivyo, Valentine huadhimishwa Februari 14 na baada ya siku hiyo, maisha yanaendelea. Lakini kwa TotalEnergies, maadhimisho yanaendelea na kutoa zawadi za Valentine hadi Februari 27. Ukienda kituo chochote cha TotalEnergies kuweka mafuta au kununua chochote katika maduka ya Bonjou, lazima utaondoka na zawadi yako ya upendo.

Sasa turudi kwenye maana halisi ya Valentine. Kama nilivyoeleza ni sikukuu ya kuonyesha upendo halisi wa kweli wa kutoka moyoni na si kuonyeshea upendo ili watu waone kuwa unapenda. Kuna tofauti kati ya kuonyesha upendo na kuonyeshea upendo.

Konyesha upendo ni ile hali ya kumwonyesha umpendaye upendo halisi wa kweli kwake ulio ndani moyoni mwako. Upendo wa kuonyeshea ni ule upendo wa kufanya vitu ili watu waone kuwa unapenda. Upendo halisi wa kweli wa kutoka moyoni, hukaa moyoni mwa mtu. Upendo huu si lazima uonekane maana mahali pa upendo huu ni ndani ya moyo wa mtu ambapo hakuna anayeweza kuuona.

Upendo wa kuonyeshea ni vile vitendo vya mtu kufanya jambo au kuonyesha ishara fulani kuonyesha kuwa unao huo upendo ili watu waone. Tatizo la kuonyeshea ishara ya upendo, mara nyingi ni ishara tuu au mapenzi, kupeana zawadi za upendo, maua, 'chocolates' au zawadi zozote za upendo ili anayependwa aone kuwa anapendwa kwa vitu vya kuonekanika lakini si lazima awe anapendwa kweli.

Kwa kadri siku zinavyokwenda, mapenzi kati ya wapendanao yamekuwa mambo ya maonyesho zaidi ili watu waone na si mapenzi ya dhati. Mapenzi ya sasa ni mapenzi ya kupenda vitu kuliko utu, hivyo mtu kujiona unapendwa ni lazima upewe vitu vya kuonekanika kama vile pesa, zawadi na mtoko ili tu kuonyeshea kuliko ukweli halisi. Naomba kutumia maneno ya lugha ya Kiingereza yasemayo "life and love is more materialistic than realistic".

Binadamu tumejaliwa uwezo tofauti wa kujieleza kwenye mapenzi. Nakumbuka enzi za ujana, nikiwa nasoma Shule ya Sekondari ya Wavulana Ilboru, Arusha, ni kawaida shule za wavulana kuwa na uhusiano ya kutembeleana na shule za wasichana watupu. Ikatokea kwa wakati huo, mkoa wa Arusha hakukuwa na shule za wasichana, hivyo Mkuu wa Shule yetu wa enzi hizo,

Mwalimu Mushi ( tukimuita kwa jina la utani Bino) akaamua wavulana wa Ilboru, watacheza muziki na wasichama wa Shule za Sekondari Weruweru, Machame na Kibosho Girls pekee za Moshi. Hizo ndizo shule wakati huo zilizokuwa na hadhi na nidhamu ya kuchanganyika na Ilboru.

Baada ya kucheza muziki, wiki zinazofuatia ni mvua ya barua za mapenzi kumiminika toka kwa wasichana wa shule hizo kuja shuleni kwetu. Ikatokea tu mimi ni mmoja wa vijana tuliofahamika kuwa ni wepesi wa kujieleza, hivyo barua hizo za mapenzi kuletwa na mimi kuzisoma na ku-draft majibu ya barua hizo kwa ustadi mkubwa, kiasi kwamba barua hiyo ikifika inakokwenda, yule binti hawezi kabisa kuchomoa. Ananaswa na maneno matamu kama samaki kwenye ndoano! Kutokana na hali hiyo, najikuta na mzigo wa barua za watu, hivyo tukajikuta tumetengeneza uhusiano wa kudumu na kiukweli baadhi ya uhusiano huo uliishia kwenye ndoa, mimi mwenyewe nikiwa mmoja wao.

Barua zile hazikuwa za maneno ya mapenzi ya kweli kutoka moyoni mwa aliyeandika kwa sababu anakuwa ameandikiwa lakini msomaji alikuwa anajisikia raha ya kweli. Aliamini hayo ni maneno ni ya kutoka moyoni mwa mwandishi kumbe alikuwa anadanganywa tu. Mapenzi ya siku hizi kudanganyana ni kwingi kuliko mapenzi halisi. Madada zetu wa kisasa nao ndio kabisa, badala ya kupenda pendo la kweli, wanapenda vitu, pesa, magari, vizawadi vidogo vidogo na starehe kuliko mapenzi halisi na ya kweli.

Moja ya mifano mizuri ya upendo wa kweli wiki hii ni nchini Tanzania ni wa picha ya pamoja ya wale Watanzania wawili waliokutana Brussels, Ubelgiji kwa mazungumzo mafupi. Ule ndio upendo wa kweli ambao unatibu na kuliponya taifa. Hongera Mama kwa upendo huu.

Kutokana na uzungu mwingi wa upendo wa kuonyeshea siku ya Valentine, wake zetu, wapenzi wetu, madada zetu, mabinti zetu, wamepoteza uwezo wa kubaini upendo wa kweli wa kutoka moyoni. Wamekuwa 'vichaa' na upendo wa vitu vya kuonekanika. Huu ni wehu.

Mmoja wa mabinti zetu wa Kitanzania ametawala mitanadao ya kijamii duniani baada ya kuweka bango kubwa la barabarani lililogharimu Sh. milioni sita likionyeshea picha ya mpenzi wake na kujieleza hivyo ndivyo anavyompenda. Bango hilo limesababisha kizaazaa kwa kila anayependwa, kutaka awekwe kwenye Bango. Bado najiuliza kwa sisi wanaume wa Kiafrika, ile kumweka tu mpenzi mmoja kwenye 'status' ya mtandao wa kijamii kunazua jambo, sasa hii ya kuweka bango itakuwaje?

Upendo ndiyo amri kuu kuliko zote Mungu aliotupa. Alisema tupendane na upendo wa kweli ni ule ukaao moyoni na si wa kuonyeshea. Kuna wanaopendwa kwa kupewa maua, zawadi, kutolewa 'out' na kufanyiwa kila kitu lakini ukawa upendo wa maonyesho tu na si upendo wa kweli. Kuna wale ambao hata kuambiwa 'Happy Valentine' hawakuambiwa, hawakupewa ua au zawadi yoyote lakini ndio wanaopendwa kweli. Pendo la kweli ni la moyoni na si la kuonekanika.

Hii ni faraja kwa wale wote ambao hamkuambiwa Happy Valentine, hamkupewa kadi wala zawadi yoyote ya Valentine. Furahini ndani ya mioyo yenu kwa sababu nyie ndio mnaopendwa pendo la kweli la moyoni ambalo halionyesheki.

Hongera TotalEnergies kuwapenda Watanzania kwa kuonyesha upendo wa kweli na si upendo wa kuonyeshea. Hongera kubwa zaidi kwa wote wanaopendwa kwa upendo mkubwa zaidi wa kweli ulioko moyoni usioonekana kuliko wale wanaopendwa kwa kuonyeshea ambao si upendo wa kweli.

**Happy Valentine wasomaji wangu**

**Nawapenda!.**

**Mob. +255 754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mwacheni Chifu Hangaya aendelee kuupiga mwingi



Na Joseph Kulangwa

SHULENI jana, leo na kesho, wanafunzi wa madarasa ya chini daima ndio huenda kuwauliza wale wa madarasa ya juu ili kufahamishwa wasichokijua katika masomo.

Hali kadhalika, wanafunzi wa shule za msingi mara nyingi ndio watawauliza wale wa sekondari, kutaka kuwaelimisha kuhusu wasichokijua. Utaratibu ni huo huo katika nyanja mbalimbali za maisha.

Ndiyo sababu pia watoto hutarajia kuwauliza wazazi wao kuwafahamisha na kuwaelekeza kama si kuwaelimisha kile wasichokijua. Ni utaratibu tu wa maisha.

Sijapata kusikia au kuona mwanafunzi wa darasa la saba, akaenda kumwuliza mwanafunzi wa darasa la tatu au la nne kuhusu masomo kwani alishayapitia na ndiyo sababu yuko juu.

Ukimwona mwanafunzi wa chuo kikuu anakwenda kumwuliza mwanafunzi wa kidato cha tano au cha sita kuhusu Kemia wakati naye anasomea Kemia Chuo Kikuu, basi ujue hapo pana mushkeli.

Ni utaratibu tu wa kimaisha ndio unaofanya watu wanapeana nafasi hizo, wala si dharau hata kidogo, hivyo aliyetangulia katangulia na anakuwa na uzoefu kuliko aliye nyuma.

Inatokea hata katika maisha ya mataifa duniani, msimwone Chifu Hangaya anahangaika huko mataifani kuzungumza na Wazungu na kuingia mikataba mbalimbali. Huko kaenda kuuliza asichokijua na kuelezwa jinsi kitakavyomsaidia.

Tulipata kuwa na Chifu huko nyuma ambaye alikuwa darasa la tatu, lakini asiyetaka kwenda kumwuliza wa darasa la saba ili kumwelimisha na kuona jinsi taaluma ya aliyemtangulia inavyoweza kumsaidia.

Chifu huyo yeye alikuwa kila mara akisema "watakuja tu" kwamba wao ndio waje kumwuliza maswali ya darasa la tatu wakati wao wako darasa la saba. Kweli inafaa hiyo au jeuri na kibri?

Mnakumbuka nyie Watanzania jinsi tulivyokuwa tunazuiwa kwenda nje ya nchi kufuata maendeleo na kuambiwa hatuendi ila wao Wazungu watatufuata, huku tukijua kuwa kimaendeleo hatuwafikii?

Nani atakataa kuwa miaka sita hivi iliyopita hatukuwa tunahitajika kwenda ughaibuni kwa kuchelea eti kutumia vibaya fedha za umma. Tukiambiwa kuwa ili uende ughaibuni lazima iwe shida kwelikweli na tena kwa ruhusa kutoka Jumba Jeupe!

Tulikuwa tukifa na tai shingoni na matatizo yetu, tukijigamba kuwa si tu matajiri hivyo hatubabaishwi na ngozi nyeupe na kama tuna shida ya kuwaona waje wao! Hivi kweli wana shida kiasi cha kututafuta au sisi ndio tuwatafute?

Hivyo mkiona Chifu Hangaya yuko huko msianze maneno yenu ya kumpachika majina ya Vasco da Gama kama mlivyomfanya Mzee wa Msoga mpaka alipokuleteeni 'chuma' kikakubondeni kichwani mkaweweseka.

Mnakumbuka mlipofikwa na UVIKO-19 mkaambiwa hakuna kukimbilia chanjo za ughaibuni kwa kuwa wazungu hao wanataka kutuangamiza kwa dawa zao tusizozijua na badala yake tujifukize? Mnakumbuka?

Bila shaka mnakumbuka tulivyoanza kuteketea mmoja mmoja kutokana na UVIKO-19 huku tukikimbilia nje kwenda kunywa midawa tusiyoijua na hatimaye kurudi na makasha kedekede ambayo hata hatujui yalikoishia.

Binadamu ukitambua udhaifu wako na kuukubali ndipo unavyoweza kutafuta na kupata ufumbuzi wake, lakini ukijifanya kijogoo na kujificha chumbani huku ukigugumia na kujifanya uko imara utaishia kuumbuka.

Hiyo ni sawa na kuvaa suti nzuri kwa nje, lakini ndani umevalia shati lililotoboka mgongoni. Unaficha udhaifu kwa maumivu yako mwenyewe. Kiko wapi sasa, hatuendi watakuja tu, tungeumbuka kama Chifu Hangaya asingekubali chanjo kutoka Marekani na Uchina.

Pamoja na kwamba sisi ni taifa huru, bado hatuna budi kukubali ni wapi mkono haufiki na kuomba kusaidiwa na wenye mikono mirefu kama ambavyo Hangaya anajaribu kufanya hivi sasa, kwa kwenda mataifa rafiki na kujieleza ili kusaidiwa.

Hata mataifa makubwa nayo huombana misaada na kusaidiana, sembuse sisi mataifa madogo tunayoendelea? Kutamba kuwa sisi ni taifa huru na wanaotaka kutusaidia, watakuja tu haina maana na ndiyo sababu mambo mengine hukwama kwa kibri tu kisicho na maana.

Tumwache Chifu Hangaya aendelee kutuwakilisha huko ughaibuni na kuja na ufumbuzi wa matatizo yetu na jambo jema analolifanya ni la kila anachokipokea anakiweka mezani tunagawana, tunanunua mahitaji yetu ya kila siku. Bila shaka mnakumbuka zile trilioni moja za UVIKO-19.

**Alamsiki!**

# Shule yafuta adhabu ya viboko kwa wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Sekondari St. Mary's, Mbezi Beach mkoani Dar es Salaam, imejivunia kuongezeka kwa hali ya nidhamu kwa wanafunzi wake hali iliyosababisha kuondoa kabisa adhabu ya viboko.

Hayo yalisemwa jana na Makamu Mkuu wa shule hiyo, Balele Rajab, wakati akizungumza kwenye kikao cha wazazi shuleni hapo na hafla ya kuwatunuku wanafunzi 51 waliofanya vizuri kwenye matokeo ya kidato cha pili mwaka jana kwa kupata daraja la kwanza.

Alisema nidhamu na mafanikio ya kitaaluma ni kama mapacha, hivyo baada ya kuweka misingi ya nidhamu, shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri kwenye matokeo ya kuanzia kidato cha pili, cha nne na cha sita kwa kupata daraja la kwanza, la pili na daraja la tatu.

"Ndugu wazazi mkisikia shule inafanya vizuri kwenye matokeo ya kitaaluma basi mjue kwenye nidhamu wako vizuri pia. Vile vile ukisikia shule inafanya vibaya sana ukichunguza utabaini wanafunzi hawakuwa na nidhamu. Sisi tumejitahidi sana kwenye nidhamu tuko vizuri," alisema

Alisema kutokana na jitihada za walimu wa shule hiyo, shule imefanikiwa kupata wanafunzi 15 wa daraja la kwanza kwenye matokeo ya kidato cha nne mwaka 2020 na kupunguza idadi ya wanafunzi wanaopata 0 huku akiahidi kwamba wanafunzi wataendelea kufanya vizuri kwenye mitihani ijayo.

Alisema ushahidi wa kazi kubwa inayofanywa ni mtihani wa utahimilifu (Mock) mwaka huu kwa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo wanafunzi 54 wa shule hiyo walipata daraja la kwanza na hakukuwa na mwanafunzi hata mmoja aliyepata 0.

"Ukiona vyaelea vimeundwa haya matokeo mazuri yanakuja kutokana na jitihada kubwa zinazofanywa na walimu wa shule hii ambao wanatumia muda mwingi sana kufundisha. Na kwa kazi kubwa tunayofanya mwaka huu mkisikia tumeingia kwenye 10 bora kitaifa msishangae," alisema

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo, Dallas Mhoja, alisema taaluma shuleni hapo imekuwa ikiboreka mwaka hadi mwaka na aliwaomba wazazi waendelee kuiamini shule hiyo kwani watoto wao wako kwenye mikono salama.

"Wazazi msiwe na wasiwasi mmechagua sehemu sahihi ya kupeleka watoto wenu, matokeo yetu yamekuwa yakiendelea kuwa juu mwaka hadi mwaka na ushahidi upo hata kama mkitaka angalieni kwenye mitandao na tunawaomba muwe mabalozi wetu kwa kusema mazuri tunayoyafanya," alisema

Alisema ili shule iendelee kufanya vizuri kunahitajika ushirikiano baina ya pande zote tatu yaani kutoka kwa walimu wa shule, wanafunzi na wazazi wao na kwamba iwapo watakwenda kwa mtindo huo shule itafika mbali zaidi.

# Tanzania, Qatar kukuza fursa za ajira

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imekusudia kuendeleza uhusiano uliopo kati yake na Qatar, sambamba na kukuza uhusiano wa kibiashara, uchumi na fursa za ajira.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema hayo juzi alipofanya mazungumzo na ugeni kutoka Qatar, katika kikao kilichofanyika jijini Dar es Salaam.

Ndalichako alisema Tanzania na Qatar zimekuwa na uhusiano mzuri kwa muda mrefu na mataifa hayo yamekuwa yakishirikiana katika mambo mengi yakiwamo biashara na uwekezaji ambayo yamekuwa na manufaa kwa pande zote.

"Nipongeze Qatar kwa kuonyesha dhamira ya dhati katika utekelezaji wa makubaliano tuliyoingia tangu mwaka 2014 ambayo yamelenga kuimarisha uhusiano wa nchi zetu katika nyanja mbalimbali zenye maslahi ya pande zote mbili," alisema.

Prof. Ndalichako alisema tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani amekuwa akionyesha dhamira ya dhati katika kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na mataifa mengine na pia amekuwa akifungua fursa za uwekezaji nchini, ufanyaji wa biashara sambamba na kuwezesha Watanzania kushirikiana na nchi marafiki katika nyanja mbalimbali.

Wakati huo huo, Waziri Ndalichako alipongeza Qatar kwa kuwa wenyeji wa Kombe la Dunia, hivyo alitumia fursa hiyo kuhamasisha ushirikishwaji wa vijana wa kitanzania katika fursa mbalimbali za ajira zitakazotolewa kuelekea katika maandalizi ya michuano hiyo.

"Tunafahamu mwaka huu Qatar itakuwa mwenyeji wa michuano ya Kombe la Dunia, hivyo mtambue kuwa nchi yetu imeendelea kuwaandaa vizuri vijana wake ili kuwa na ujuzi ambao unahitajika katika nyanja mbalimbali ambao utawawezesha kuajirika," alisema.

Sambamba na hayo, Ndalichako alisema serikali imeendelea kuratibu vyema na kuzingatia misingi katika kupeleka watanzania kufanya kazi katika maeneo mbalimbali ya nje ya nchi.

Pia alisema serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikiratibu Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi ambayo imekuwa chachu ya kuzalisha wataalamu wenye ujuzi wa fani mbalimbali zinazohitajika nchini na kwenye mataifa mengine.

Naye, Katibu Mkuu kutoka Wizara ya Kazi Qatar, Mohamed Hassan al Obaidali, alieleza kuridhishwa na mazingira yaliyopo nchini na ukarimu wa Watanzania na kuahidi kuwa nchi hiyo itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuangalia uwezekano wa kuwekeza kwenye miradi ya kiuchumi itakayoziletea maendeleo nchi hizo mbili.

## DARASA LA NDOA

# JE, FEDHA NI BARAKA AU LAANA KATIKA FAMILIA?



**Na Mch.Dk. Enock Mlyuka**

KUMEKUWA na mitazamo tofauti kuhusu fedha kaika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Mitazamo hiyo imetokana na uhitaji au athari chanya na hasi kutokana na rasilimali hiyo.

Fedha ni njema na mtu kuwa nayo si uovu wala dhambi lakini nafasi unayoipa katika maisha yako ndiyo itakayoamua kama ni baraka au laana. Fedha ni baraka ikitafutwa kwa halali na kutumika vizuri kwani inaweza kuwa nyenzo ya kuleta maendeleo pale itakapotumika vizuri kwa mambo yenye manufaa. Hata hivyo, fedha inayo uwezo wa kuleta maumivu na kugeuka kuwa shina la ubaya isipotumika vizuri.

Rasilimali hii iitwayo fedha, ina nguvu katika maisha ya mtu binafsi na katika uhusiano na watu wengine. Ziko baadhi ya ndoa zilizoimarika baada ya kupata fedha na wanandoa kufurahia mafanikio yatokanayo na fedha zilizopatikana. Lakini ziko pia ndoa zilizoharibika baada ya fedha kuingia. Baadhi ya wanandoa hawafurahii maisha ya ndoa pamoja na kwamba wanazo fedha. Fedha imegeuka kuwa kirusi kinachoharibu ndoa na uhusiano wa wanandoa.

Utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa migogoro mingi ya wanandoa hutokana na mambo yanayohusu fedha. Matumizi ya fedha yamesababisha matatizo mengi katika ndoa nyingi. Ubinafsi umezielemea ndoa nyingi.

Tatizo linakuwa kubwa hasa pale ambapo fedha ya mume inapoonekana haimhusu mke, hivyo mke kutokutakiwa kuhoji au kuchangia mawazo yoyote juu ya matumizi ya fedha. Hali kadhalika, wako baadhi ya wanawake ambao hufanya vivyo hivyo dhidi ya waume zao.

Mfumo dume katika jamii umeongeza ukubwa wa tatizo hili kwani katika maeneo mengi suala la fedha ameachiwa mume bila mke kuwajibika, kujua au kuchangia lolote. Wanawake wenyewe wengi wao wamewaachia waume zao kuwajibika kwa kila kitu kinachohusu fedha na katika uamuzi wowote unaohusu fedha ndani ya ndoa. Pia uamuzi mwingine umeangamiza familia kwa sababu ni mtu mmoja, yaani, mume au baba tu katika ndoa ndiye hutoa uamuzi kuhusu mambo yanayohusu fedha.

Ni ukweli ulio dhahiri kwamba katika zama hizi mambo yamebadilika.

Wanawake wengi wana uwezo wa kifedha kwani wanafanya kazi, biashara na kuingiza pato katika familia na ndoa. Uzoefu unaonesha kuwa, ziko baadhi ya familia ambazo mke ndiye mwenye kipato kikubwa kuliko mume. Hali hiyo imesababisha familia nyingi siku hizi kutunzwa na wanawake, hivyo kusababisha baadhi ya kinababa kujisikia duni kwa wake zao (inferior) kiasi cha kupoteza hali yao ya kujiamini (lose confidence).

Kwa kiasi kikubwa, suala la fedha limeleta matatizo katika ndoa nyingi za leo. Imetokea kwamba wanandoa waliishi kwa amani kabla ya fedha kupatikana au kufanikiwa kimaisha. Lakini baada ya kupata mafanikio, wanandoa wamebadilika na kuanza kuumizana.

Hatua hiyo imesababisha thamani ya mwenzi kupotea. Mwenzi anaonekana ni mtu asiyeendana na hadhi ya mwenzake. Fedha imependwa zaidi kuliko mwenzi au familia. Hali ya namna hii imesababisha kwa sehemu kubwa baadhi ya wanandoa kutengana na ndoa kuvunjika.

Kutokana na hali hiyo ya kusambaratika au kuvunjika kwa ndoa, athari zake ni kubwa si kwa wanandoa wenyewe tu, bali kwa watoto waliozaliwa katika ndoa hizo. Watoto huathirika kiroho, ki-saikolojia, na ki-makuzi. Wanakosa haki ya kuishi na wazazi wao kwa pamoja, wanakosa malezi bora ya baba na mama, wanakosa furaha na kujisikia kutokuwa salama (insecure) kwa sababu ya kukosekana kwa baba au mama.

Watoto wanarithishwa ubaya ikiwa ni pamoja na roho ya kuoa, kuacha na kuachika.

Kwa upande mwingine, Fedha huleta mhemko. Baadhi ya wababa wakipata fedha ndiyo mwanzo wa kufanya vitendo vya ukatili katika familia (domestic violence) na unyanyasaji (harassment) kwa wake zao. Uhusiano mpya huanzishwa nje ya ndoa (michepuko) ambako fedha hupata matumizi makubwa zaidi huko nje kuliko katika familia yake. Hali hii hufisha uhusiano wao na kudumaza ustawi wa ndoa na familia.

Hali kadhalika, wako baadhi ya wanawake ambao wakifanikiwa na kuwa na kipato kikubwa kuliko waume zao, kiburi na dharau huinuka dhidi ya wenzi wao. Mahali pengine, mume huishi kama kibarua au mkimbizi ndani ya nyumba yake. Kauli mbaya za mke kwa mumewe huwa jambo la kawaida.

Mke hutumia fedha anavyotaka na kufanya mambo anavyojisikia binafsi bila kumshirikisha mumewe. Akiulizwa anasema hii ni pesa yangu haikuhusu kwani ninao uhuru wa kuitumia nitakavyo.

Matokeo yake, heshima kwa mume hupungua kama si kuondoka kabisa. Mbaya zaidi, baadhi ya wanawake husahau kutimiza majukumu yao ya kindoa kwa waume zao. Mazingira kama haya yamesababisha hatima na mustakabali wa ndoa nyingi kuwa katika mashaka makubwa.

**●Mch. Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

FEBRUARI 20, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




Ukurasa 14


## MPE MTOTO WAKO Uji wa mchele, uliochanganywa maboga



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Namna ya kupamba mitungi ya maua ya asili




## KATUNIKA

Ukurasa 16

# MATITI YALIYOSIMAMA


## Mayai, barafu hukurudishia furaha




Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA










## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
INA, UNA, PANDE, ZIBIA, IKINGE, ZENGEA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa nyumbani akimsaidia kazi za ndani mama yake. Wakati akiendelea na kazi zake, mama yake alimwambia akasafishe birika ili waandae chai ya kunywa asubuhi.

Juma alikwenda kabatini akalichukua birika na kisha kujaza maji ya kwenda kuyaweka jikoni. Wakati akielekea jikoni alimuuliza mama yake.

Juma: Mama eti birika lina mikono?

Mama: Si huo ulioushika juu ya birika ndio wanauita mkono

Juma: Mbona mwalimu alituambia tusiwe na mikono ya birika kwa nini?

Mama: Mwanangu mwalimu wenu alitaka muwe watu wa kijitoa na sio kuwa mabahili kwani watu wasiokuwa na tabia ya kutoa huitwa mikono ya birika.

SWALI

Paa yupo katika jamii gani ya wanyama wa porini?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Nguvu za giza zilivyopindisha hatima ya watu wengi

KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze mada niliyoianzisha wiki iliyopita. Nilisema magumu ambayo wengi wanapitia hayakujileta bali yamesababishwa na nguvu fulani isiyoonekana kwa macho ya kawaida.

Nilijadili wasomaji wawili wa safu hii kupitia ujumbe walionitumia kuhusu changamoto zinazowasibu, hivyo kuhitaji msaada wa ushauri. Mmoja ni mume mwenye mke na watoto wawili ambaye alikuwa anafanya kazi zake vizuri, lakini ghafla akabadilika.

Akaanza kukataa chakula, hataki kuoga, kupiga mswaki, hataki kutoka nje ya nyumba yao na kibaya zaidi anaogopa watu wakiwemo wana familia yake. Amekuwa kwenye tatizo hilo takriban miezi sita. Ndipo akakimbilia watumishi wa Mungu kutafuta msaada wa maombezi baada ya matibabu hospitalini kutompatia nafuu.

Kijana mwingine niliyemjadili alijitambulisha kwa jina la Anthony anayeishi Zanzibar kikazi. Huyu katika ujumbe wake alisema ni miaka saba sasa mambo yake hayaendi tangu amalize kidato cha nne na alipata divisheni 'one'.

Alisema kwa sasa ana umri wa miaka 26 anajitahidi kwa kila hali lakini haoni mwanga. Kidato cha tano alisoma vizuri masomo ya sayansi (PCM) lakini wiki moja kabla ya mitihani akawa anaugua ugonjwa wa ajabu uliosababisha ashindwe kusoma hata kufanya mitihani yenyewe.

Matokeo yake hakufanya vizuri. Akachukua diploma ya udaktari lakini napo ikawa ni kuugua vile vile, kiasi cha kumkatisha tamaa. Hata hivyo, alijitahidi akafaulu kawaida ingawa angeweza kupata daraja la juu zaidi.

Ugumu ukaendelea katika kupata kazi yenye kipato cha kuinua maisha yake. Huo mshahara mdogo aliokuwa akipata haukai. Mipango mizuri na fursa anapata lakini kabla ya kuzifanyia kazi linaibuka jambo, anapoteza fursa zote. Anabaki anajiuliza, kuna tatizo gani?

Mpenzi msomaji, mara nyingi nimeeleza hapa kwamba yapo mambo yanawasibu watu wengi wasijue kwamba kipo kisababishi kilichojificha. Ziko roho zinawaangusha watu kwenye nafasi zao au hata kuwachelewesha katika kufikia hatma za maisha yao.

Kwa mfano, kucheleweshwa katika elimu ambayo ni ufunguo wa maisha kama ilivyotokea kwa Anthony. Wapo waliocheweshwa pia kuzaa watoto, kuolewa au kuoa, kufanikiwa kibiashara na hata kupandishwa vyeo kazini.

Kucheleweshwa huku kumewaumiza wengi ndiyo maana hata Mungu mwenyewe akaweka wazi kwenye Neno lake kwamba, "kilichotarajiwa kukawia kuja, moyo huugua, bali haja ya mtu ikipatikana, ni mti wa uzima".

Watu wengi mioyo yao imeugua. Hawana amani kwa sababu walichokitarajia kwa miaka mingi kimechelewa. Mambo ambayo wangefanya kwa mwezi mmoja, inachukua miezi sita au zaidi!

Wengine walipaswa kujenga nyumba zao kwa miaka miwili lakini hadi sasa ni miaka mitano bado hawajamaliza. Wengine, kwa elimu waliyo nayo, walipaswa kupandishwa vyeo, lakini sasa ni miaka 10 bado wako pale pale.

Ulipaswa kuoa au kuolewa ukiwa na umri wa miaka 25, 26 au 27 lakini sasa ni miaka 40 hujaolewa au kuoa. Watu wa aina hii, mara nyingi hawana amani kwani walivyotarajia vimechelewa. Na chanzo kikuu cha kuchelewesha miujiza yetu ni shetani na mawakala wake (mapepo, mizimu, majini, wachawi). Isitoshe, watu wengi sana wametolewa kwenye nafasi zao nzuri kwa nguvu za kichawi. Kwa kutojua kuna uchawi ni hatari sana!

Wako watu wamedanganywa kuwa hakuna uchawi, hivyo wakajiachilia wala hawana muda wa kutafuta siri za kuwachelewesha ili kuzishinda hizo nguvu za kichawi.

Wengine wamepokonywa nafasi na mizimu. Haya ni mapepo yanayotawala koo, familia, miji na hata nchi. Ni mapepo yenye nguvu sana kwenye maisha ya watu wengi. Ni kwa sababu mababu wa zamani waliyapa nafasi kuyaabudu na kuyaomba, kisha kuyapa kila kitu yalichotaka kutoka kwao.

Yamkini watu wengi leo wanaadhibiwa kwa sababu Mungu alishatoa onyo pale aliposema katika neno lake kwamba, "Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nchi ya utumwa, usiwe na miungu mingine ila mimi".

***Mpenzi msomaji, bila shaka umejifunza jambo hapo. Kumbuka, roho ya kuchelewesha ni kizuizi kikubwa katika kufikia hatma ya maisha yetu. Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Jiji Dodoma kuweni wabunifu eneo hili linatia kinyaa

ENEO la kando ya barabara ya Dodoma hadi Morogoro jijini Dodoma, linashangaza kama liko ndani ya jiji hilo ambalo ni makao makuu ya nchi.

Kabla, lilikuwa linatumiwa na wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, lakini kwa sasa limebaki wazi likibaki kuwa mazalia ya mbu na makazi ya wadudu wengine.

Eneo hilo linatazamana na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) ikiwa ni hatua chache kutoka makutano ya barabara hiyo na barabara ya Singida na mita chache kutoka Bungeni, taasisi ambayo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi.

Kwa sasa kila inapofika asubuhi na jioni, mabasi kutoka mikoa mbalimbali yanaegeshwa kushusha abiria na mizigo mbalimbali. Haliko mbali sana na hoteli na nyumba ya kulala wageni ambazo wageni wengi wanaofika jijini hapa hutembelea.

Kwa sasa ni msimu wa mvua, kuna madimbwi makubwa ambayo yamekuwa mazalia ya mbu na wadudu wengine. Pana mwonekano mbaya, pachafu, hakuna miti wala maua kiasi cha kujiuliza kweli Jiji la Dodoma limeshindwa kufanya eneo hilo lionekane safi na la kuvutia?

Ni aibu kwamba unatoka kwenye Bunge la Watanzania ambalo linapitisha bajeti ya nchi na kujadili mambo mengi makubwa kwa ajili ya hatima ya nchi, unakutana na eneo lenye kutia kinyaa.

Eneo hilo linakwenda hadi karibu na makutano ya barabara ya Shabby na hoteli kubwa ambazo hupokea wageni wa kimataifa kwa ajili ya mikutano mikubwa.

Pia lina ofisi nyingi za mabasi mengine ambayo humalizia safari hapo lakini lina madimbwi makubwa kiasi cha kujiuliza viongozi hawaoni? Ni mahali ambapo pangepandwa miti na maua ya kuvutia.

Eneo hilo ambalo ni nje ya hifadhi ya barabara, lingeweza kutumika vizuri kuwa kivutio cha jiji hilo kwa kuwa liko jirani na Bunge lakini limeachwa linazalisha mbu na wadudu wengine ambao ni hatari kwa afya za binadamu.

Eneo hilo kuna kituo cha Daladala cha CBE ambacho hufurika wasafiri wa mikoani na ndani ya Dodoma. Asubuhi kuna daladala, pikipiki, teksi na bajaji lakini hali si ya kuridhisha kabisa.

Ni lazima watendaji Jiji la Dodoma watafakari eneo hili kwamba kupitia vikao vya Baraza la Madiwani, linaweza kuibuliwa kama chanzo cha mapato ikiwa kutakuwa na ubunifu, lazima ligeuzwe kuwa fursa na siyo chanzo cha magonjwa.

Mfano kama wangeruhusu majengo ya muda mfupi mazuri kwa ajili ya abiria kupata chakula au mahitaji mengine wangepata kodi ya halmashauri pia, maadam ingekuwa ya kuvutia kila mmoja.

Kama wanaona haiwezekani kuliendeleza kwa ushirikiano na sekta binafsi basi litengenezwe kwa kiwango cha kuridhisha kuliko hali ilivyo sasa. Kwa mtazamo wangu, kwa sasa eneo hili lina aibisha nchi.

Bunge hutembelewa na wageni mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ambao lazima wapite eneo hilo kama wanatumia usafiri wa barabara. Hata wakitumia ndege kama hoteli zao za kufikia ziko maeneo ya Kisasa na kwingine uelekeo wa Chamwino, maana yake lazima wapite hapo na kuona madimbwi makubwa makubwa.

Ni muhimu sana watendaji wa manispaa na halmashauri kuwa wabunifu hasa kwenye vyanzo vya mapato, kuweka mandhari ya jiji yenye kuvutia badala ya hali iliyopo sasa ambayo mtu analazimika kukwepa madimbwi makubwa ya maji.

Lazima kuwe na utaratibu wa kusimamia usafi na kulipanga jiji ili liwe na ubora unaotakiwa pia kijifunza kwenye majiji mengine duniani ambayo karibu na Bunge lao kumetengenezwa kuwa kivutio kizuri na si hali ya uchafu kama eneo hilo lilivyo.


Japo kwa uchache nje ya Bunge la Ethiopia, Uganda, Kenya, Zambia, Zimbabwe, Afrika Kusini, Denmark, Sweden na Marekani ni maeneo yenye kuvutia, yenye miti na maua mazuri, kwetu kumezungukwa na majengo chakavu, machafu na yasiyoridhisha jambo ambalo si sawa kabisa.

Kama wengine wameweka maeneo yao safi muda wote ambayo yamezungukwa na maua mazuri ya kila aina, kwa nini Dodoma inashindwa kupanda miti na maua ya kuvutia eneo hilo hasa kwa wakati huu wa mvua.


Tumieni mvua zinazoendelea kunyesha kupendezesha maeneo mengine au ruhusuni watu binafsi wapande miti na maua kama inavyofanyika Dar es Salaam kiasi cha kuwafanya wapate kipato na wapendezeshe Jiji.



Moja ya vionjo vya harusi ni taji linalovaliwa na bibi harusi kichwani. Hapa tunakuletea aina mbalimbali ya mataji ambayo yanapendeza kuvaliwa wakati wa kufunga ndoa.







# MITINDO

Na Christina Mwakangale



# POLO 'SLEEVE' NDEFU
# Mashati yanayowadatisha vijana

WAKATI unakwenda kasi, kila kitu kinabadilika na kuwafanya watu kuishi maisha ya kisasa zaidi.

Moja ya sehemu ambayo watu wanapitia katika mabadiliko hayo, ni mitindo ya mavazi iwe ya kiume au ya kike yanazidi kuwa tofauti kutokana na ubunifu na ubora wake.

Vazi la shati aina ya Polo ni moja ya nguo za kisasa ambazo zinapendwa na vijana kuvaliwa kutokana na mwonekano wake kuwa mzuri.

Mashati ya polo 'sleeve' ndefu kwenye vazi lako yatakuletea kipimo kizuri cha mtindo katika msimu wowote wa mwaka.

Hii ni baadhi ya mitindo ya mashati ya Polo yanayopendwa zaidi kuvaliwa na watu wa aina mbalimbali.

**BOGLIOT**

Yana ubora zaidi na mikono mirefu, yana sifa ya kuwa kitambaa chepesi . Ina sifa ya kutosha vyema mwili, mikono na vifungo na kuoneka nadhifu zaidi.

**BOTTEGA VENETA**

Ni nzuri pale unapovaa hasa ukiweza kuchagua rangi. Wabunifu wameitengeneza kinadhifu zaidi hasa unapoivaa kwa kuonyesha vema viungo vyako.

Mashati haya ya polo yanapendeza kama ukichagua rangi ya bluu, khaki na samawati.

**BRINELLO CUCILLI**

Ina mwonekano mzuri kutokana na urefu wake, kitambaa kizito kiasi na chenye kuonyesha uhalisia wa umbo lako.

Hapa huna haja ya kuchagua rangi kwani mtindo wake pekee unatosha kuupendezesha mwili na kuonekana maridadi.

URAMBO

URAMBO

Na Mary Geofrey

# MATITI YALIYOSIMAMA

## Mayai, barafu hukurudishia furaha



IDADI kubwa ya wanawake wanapoteza furaha pale wanapoona baadhi ya viungo vyao vimepoteza mwonekano wa kupendeza kutokana na sababu mbalimbali.

Matiti ni moja ya kiungo ambacho kinamuelezea mwanamke jinsi alivyo, kuanzia umri na hata mtindo wake wa maisha. Kutokana na umuhimu wake wanaweka umakini katika kuyatunza ili kubaki katika hali bora kila wakati.

Kumekuwepo na wanawake ambao wanapenda matiti makubwa na yaliyosimama vyema kama bado wasichana.

Lakini kwa bahati mbaya, jambo hilo haliwezekani kwa sababu umri umewatupa mkono au kuzaa yamelala na kupoteza mvuto wake.

Hata hivyo, wale ambao wanahitaji kurudi katika ujana, kuna njia ambazo ukizifuata unarejesha furaha yako ya kuwa na matiti yaliyosimama.

**MAZOEZI**

Kama matiti yako yamelala unaweza kufanya mazoezi maalumu ya kusisimua misuli iliyolala.

Mazoezi ya aina hiyo huimarisha misuli na kuboresha afya ya ngozi yako na kusababisha matiti kuwa na nguvu kama zamani.

**MASAJI YA BARAFU**

Chukua kipande cha barafu na kisha unajichua taratibu kuzunguka matiti yote.

Aina hii ya uchuaji ukifanya kila mara inasaidia kuimarisha misuli na kuwezesha kurudi kama ilivyokuwa awali.

**MAYAI**

Mchanganyiko wa mayai, vitamin E na maziwa ya mtindi unasaidia kukurudisha katika matiti ya ujana.

Paka kama unajichua wakati wa kulala kila siku utaona unapata matokeo mazuri.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# MPE MTOTO WAKO

## Uji wa mchele, uliochanganywa maboga

KAMA tunavyofahamu boga ni aina ya tunda lenye madini mengi ambayo yana faida kubwa katika mwili wa binadamu

Ndani ya boga kuna madini kama zinki, kopa, magnesium, chuma , manganese na phosphorus ambayo husaidia uzalishaji wa maziwa kwa mama anaenyonyesha.

Kutokana na kuwa na utajiri wa madini, ni chakula kizuri kwa watoto hasa ukichanganya kwenye uji wa mchele wenye karoti.

Mahitaji

Mchele robo, boga vipande viwli, siagi kijiko kimoja, karoti tatu, ladha ya strawberry nusu kijiko na maziwa.

Namna ya kupika

Safisha mchele, bandika jikoni weka chumvi na maji mengi. Usiweke karoti na boga mwanzoni, sababu vitaiva kabla mchele na vitaroJeka, virutubisho muhimu vitapotea.

Ukikaribia kuiva weka karoti na boga koroga. Weka butter, funika mpaka uive. Hakikisha maji yamebaki kidogo sana.

Ongeza ladha yoyote uliyonayo mimi nimeweka ladha ya strawberry koroga vizuri. Hakikisha umechanganyikana vizuri na umeiva na epua.

Andaa chombo cha kusagia, weka chakula ongeza maziwa saga. Uwekaji wa maziwa unategemea na uzito wa chakula unaotaka.

Weka kwenye bakuli, mpe mtoto ale, pia tunza kwenye jokofu, kama kitabaki na hapo utakua umemaliza.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Rembesha uzio kupendezesha nyumba yako

UZIO ni sura katika nyumba ambao unaweza kutumika kama urembo wa nyumba kulingana na mhusika anavyotaka uwe kwa kutegemea bajeti au ubunifu unaotumika kuutengeneza.

Kwa ujumla, nyumba inapozungushiwa uzio iwe ni kwa ajili ya ulinzi, usalama, faragha au mwonekano, inasaidia pia kuongeza thamani ya nyumba husika.

Kwa mazingira yetu ya Kitanzania, kuna uzio wa aina mbalimbali ukiwamo wa matofali, mbao, miti, makuti, chuma, aluminium, wavu na mabati.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Michael Samuel, anasema yako mambo ya kuzingatia kabla ya kuweka uzio wa nyumba yako.

Anasema ni vyema ukaepuka kukurupuka kuchagua uzio kabla hujafahamu gharama za utunzaji wake na kwamba endapo utaamua kimakosa, kuna uwezekano wa kuharibu mwonekano wa sura ya nyumba yako hata kama ni nzuri kiasi gani.

"Kwa mfano unapoweka uzio wa mbao, unatakiwa ujue kwamba unatakiwa kupakwa rangi mara kwa mara na ujue zinaoza pia baadaye. Kwa hiyo zinahitaji maboresho ya kila mara kwa sababu pasipo kufanya hivyo zinaharibika. Hivi ni vitu ambavyo unapswa kujua katika kila aina ya uzio unaotaka kuweka," anasema Samuel.

Jambo lingine, anasema kabla ya kutengeneza uzio wako, unatakiwa ufahamu unatakiwa uwe kwa mtindo gani.

Anashauri kwamba uzio wa kurembesha zaidi katika lango kuu ikiwamo kuweka taa za rangi, husaidia kuweka mwonekano mzuri wa ukuta na nyumba kwa ujumla.

Samuel anashauri kuweka uzio wenye kuleta faragha na wa kuimarisha ulinzi katika nyumba na si bora uzio.

Anasema kwamba uzio unaoacha nafasi au matundu katika nyumba, hauna faragha na wala hauwezi kukulinda vya kutosha ila unakupa starehe ya kuangalia kinachoendelea nje ya makazi yako unapokuwa umejipumzisha.



## Namna ya kupamba mitungi ya maua ya asili



WATU wenye nyumba kubwa na zenye nafasi wanapendelea kuzipendezesha na vitu vya asili kama mitungi ya maua ya asili, maua bandia na mapambo mengine.

Mapambo ya mitungi yenye maua asili yanapendeza zaidi kuwekwa katika maeneo mapana yenye hewa ya kutosha ili kuendelea kustawisha miti ya maua.

Leo nakupatia dondoo za kuzifuata za kuweka mitungi yenye maua asili katika sebule yako kubwa.


1: Nunua mitungi yenye rangi isiyong'aa ambayo idadi yake italingana na ukubwa wa sebule, lakini unashauriwa iwe michache ili kuweka mandhari nzuri.

2: Weka udongo wenye rutuba na ambao hautoi harufu, panda maua yako huku ukimwagilia maji machache ambayo hayataharibu maua yako.

3: Weka mitungi katika maeneo yanayoingiza hewa na mwanga kama madirishani na mlangoni.

4: Panda maua tofauti kwa kila mtungi ili iwe rahisi utunzaji wake na kufanya kuwe na mwonekano wa kupendeza.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
INAWEZEKANA YULE SIO AFISA WA TWAKUKUR! KATUTISHA TU.
NANI KASEMA?
!?
RIP
LIGI YETU
SEMA CHOCHOTE BABY HATA KUKUBEBA NITA-KUBEBA...
WAKATI HUO UWE TAYARI USHAANDIKA WOSIA UZIKIWE WAPI..
LEO MANKA KASEMA HAKO-PESHI BIA...
ACHA USHAMBA MIMI NAKOPA 'POMBE'
ALIPONIOA MKE WA PILI SIKUJUA KAMA KUNA SHUGHULI HII
LEO AFADHALI KAZIMIKIA BAR YA KARIBU
TUMEIACHA 'SINGELI' AMBAYO NDIO STAILI YETU TUMEKOMALIA MIPIANO!
SIJUI LINI NA SIE TUTARINGA NA MITINDO YETU!
TOKA MWANZO WA SAFARI PIANO TU!
KOSA LA NANI?
WAKISAPOTIWA WAKIVUKA WATA-'VIMBA' HA HAAA!
SIO KOSA LA NANI? TUNATAKA SINGELI IIGWE NA MATAIFA MENGINE...
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKITAKA KAZI YA GEREJI USIOGOPE KUCHAFUKA



Meli ya mizigo inayoitwa Felicity Ace ikiendelea kuwaka moto karibu na ufukwe wa Ureno jana. Meli hiyo imebeba magari ya kifahari yaliyokuwa yakisafirishwa kuelekea nchini Marekani. **PICHA: AFP**

# Marekani, Urusi zashtumiana mvutano unaoendelea Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden, amesema ana uhakika kiongozi wa Urusi Vladimir Putin, ameamua kuivamia Ukraine, na kwamba shambulio linaweza kutokea wakati wowote siku zijazo.

Biden alisema tathmini hiyo ilitokana na ujasusi wa Marekani, ambao ulipendekeza mji mkuu wa Kyiv ungelengwa katika uvamizi huo.

Hata hivyo, Urusi inaendelea kukanusha kuwa na mpango huo wa kuivamia Ukraine .

Mataifa ya Magharibi yanaishutumu Urusi kwa kujaribu kuanzisha mgogoro bandia katika maeneo yaliyojitenga ya mashariki mwa Ukraine ili kuipa sababu ya kuanzisha mashambulizi.

Marekani inakadiria kuwa Urusi ina wanajeshi 169,000 hadi 190,000 waliokusanyika ndani na karibu na Ukraine, idadi ambayo inajumuisha wapiganaji wanaoungwa mkono na Urusi katika Jamhuri za Donetsk na Luhansk mashariki mwa Ukraine.

Katika hotuba ya televisheni kutoka Ikulu ya White House, Rais Biden, alisema nchi yake ina sababu ya kuamini kwamba majeshi ya Urusi yanapanga na kukusudia kushambulia Ukraine katika wiki ijayo, au katika siku zijazo. "Kufikia wakati huu nina uhakika kwamba amefanya uamuzi," aliongeza, akimaanisha Rais Putin.

Lakini, alisema, Urusi inaweza bado kuchagua diplomasia na haijachelewa sana kujiondoa na kurudi kwenye meza ya mazungumzo.

Mapema Ijumaa, katika ishara nyingine ya kuongezeka kwa mvutano, viongozi wa maeneo mawili yanayotenganisha Ukraine na Urusi walitangaza kuwahamisha wakazi wao, wakisema Ukraine imezidisha mashambulizi ya makombora na inapanga kufanya mashambulizi.

Ukraine imesema mara kwa mara kuwa haipangi kufanya mashambulizi yoyote, na Waziri wa Mambo ya Nje Dmytro Kuleba, alipuuza kile alichokiita ripoti za upotoshaji za Urusi.

Denis Pushilin, Mkuu wa Jamhuri ya Watu wa Donetsk (DNR), alitangaza kuhamishwa kwa watu hao katika video inayodaiwa kurekodiwa siku ya Ijumaa.

Hata hivyo, uchambuzi wa BBC wa metadata ulionyesha kuwa ilirekodiwa siku mbili zilizopita, kabla ya kupamba moto kwa uhasama.

Ikulu ya Kremlin, ilisema Rais Putin aliamuru kambi za wakimbizi zianzishwe karibu na mpaka na misaada ya dharura itolewe kwa watu wanaofika kutoka maeneo yaliyojitenga. Vyombo vya habari vya serikali viliripoti mabasi kadhaa yaliyokuwa yamewabeba wakazi wa eneo hilo yalikuwa yakielekea Urusi.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, iliita tangazo la kuwahamisha watu kuwa ni hatua ya hila ya Urusi inayolenga kuvuruga ulimwengu kutokana na ukweli kwamba Urusi inajenga vikosi vyake katika kujiandaa kwa shambulio.

Ikulu ya White House, ilisema uhamishaji huo ni mfano wa kutumia habari potofu kama kisingizio cha vita.

Juzi, idara ya ujasusi ya kijeshi ya Ukraine ilisema kuwa imepokea taarifa kwamba vilipuzi vilitegwa katika vituo vya miundombinu huko Donetsk kwa ajili ya maandalizi ya kile kinachoitwa shambulio la uwongo.

Hapo awali, mamlaka zinazotaka kujitenga zilisema kuwa gari iliyokuwa imeegeshwa ililipuliwa karibu na jengo la serikali huko Donetsk.

Maofisa wa Marekani na Ukraine walisema lilikuwa ni shambulio lililopangwa ili kuzua hali ya wasiwasi.

Urusi imekuwa ikiunga mkono uasi wenye silaha katika eneo la Donbas mashariki mwa Ukraine tangu mwaka 2014. Takriban watu 14,000 ikiwa ni pamoja na raia wengi wamekufa katika mapigano.

Wakati huo huo, Rais Putin alisema hali mashariki mwa Ukraine inazidi kuwa mbaya.

Katika mkutano na waandishi wa habari, alitoa shutuma zisizo na uthibitisho wa ukiukwaji mkubwa wa utaratibu wa haki za binadamu na kuwekwa sheria za kibaguzi kwa watu wanaozungumza Kirusi.

Alisema bado yuko tayari kujadili mzozo huo na viongozi wa Magharibi, lakini aliwashutumu kwa kupuuza wasiwasi wa usalama wa Urusi, na akaonya kwamba mpango wowote lazima ujumuishe ahadi ya kisheria kwamba muungano wa usalama wa Nato utasimamisha upanuzi wake kuelekea upande wa mashariki.

Jana, Rais Putin aalisimamia mazoezi makubwa ya vikosi vya kimkakati vya makombora ya nyuklia ya Urusi.

# Meli ya mizigo yawaka moto baharini, magari 3,965 ya kifahari hatarini kuteketea

**LISBON,** URENO

MAELFU ya magari ya kifahari aina ya Porsche na Volkswagen yameachwa kwenye meli ya mizigo baada ya kushika moto katika Bahari ya Atlantiki wakati ikielekea Marekani.

Meli hiyo iliyopewa jina la Felicity Ace, ilikuwa ikisafiri kutoka Emden nchini Ujerumani, kabla ya kushika moto kwenye ufuo wa visiwa vya Azores nchini Ureno.

Gazeti la Ujerumani la Handelsblatt liliripoti kuwa meli hiyo ilikuwa imebeba magari 3,965, ambayo pia ni pamoja na Audi, Lamborghini na idadi ndogo ya Bentley.

Hata hivyo, wafanyakazi wa meli hiyo wameokolewa.

Jeshi la wanamaji la Ureno lilisema hakuna mtu aliyejeruhiwa na moto huo uliozuka siku ya Jumatano, na wafanyakazi 22 walipelekwa hotelini baada ya jeshi la wanamaji, meli nne za wafanyabiashara zinazosafiri katika eneo hilo na Jeshi la Wanahewa la Ureno kukamilisha uokoaji

"Mmiliki wa meli Felicity Ace, anawasiliana na wakala husika ili kuandaa mpango wa kuivuta meli, jeshi la wanamaji la Ureno lilisema katika taarifa yake.

"Hadi sasa, hakuna chanzo cha uchafuzi wa mazingira kilichorekodiwa." Taarifa hiyo ilizidi kusema.

Kwa mujibu wa Handelsblatt, barua pepe ya ndani kutoka Volkswagen Marekani, ilisema kuwa meli hiyo ilikuwa imebeba magari 3,965 ya VW, Porsche, Audi na Lamborghini.

Volkswagen haikuthibitisha idadi ya magari kwenye meli hiyo, lakini Porsche ilisema ilikuwa na takriban modeli zake 1,100 kwenye meli hiyo.

Kampuni hiyo ilisema inafahamu tukio lililohusisha meli ya mizigo ya watu wengine inayosafirisha magari ya Volkswagen Group katika Bahari ya Atlantiki.

Bentley alithibitisha kuwa magari yake 189 pia yalikuwa kwenye meli hiyo.

"Tunafanya kazi na kampuni ya usafirishaji ili kupata habari zaidi," msemaji alisema.

Meli hiyo ilikuwa ikisafiri kuelekea kiwanda cha Volkswagen huko Davisville, Rhode Island, kulingana na tovuti ya Marine Traffic.

Mteja mmoja alisema katika Twitter kuwa Porsche yake ilikuwa kwenye meli iliyotelekezwa.

## MAKALA

# TANZANIA NI MUHIMU ZAIDI KULIKO VYAMA VYA SIASA



Na Magabilo Masambu

TANZANIA imekuwa na historia yenye mfano wa kuigwa kwa miongo kadhaa katika ukanda wetu huu wa Afrika, ikitambulika kuwa nchi yenye umoja na upendo kwa wananchi wao kwa wao na mataifa mengine yanayoizunguka.

Tumekuwa na mifumo mizuri inayotufanya tujione kila wakati kwamba sisi ni Watanzania na wala si sisi ni Wajita, Wasukuma, Wahehe, Wachaga, Wahaya na kadhalika. Si jambo la bahati mbaya bali ni kwa sababu ni taifa lililojengwa kupitia elimu na uhusiano wetu wa kijamii. Tunaoleana bila kuulizana kwa sababu tunajiona Watanzania na kwamba ni wamoja.

Misingi ya namna hii inapaswa kuendelea kujengwa ili kutofanya umoja wetu kulegalega au kuvunjika kwa namna yoyote ile. Tunazo dini zetu kila mmoja licha ya kwamba serikali yetu haina dini na bado tumeendelea kuishi pamoja kwa kuheshimiana kwa imani zetu. Hatugombani wala kukosana kwa sababu ya tofauti zetu za dini na uhusiano wa namna hii umekuwapo kwa muda mrefu, hivyo hatutarajii kuuvunja.

**Hatugombani wala kukosana kwa sababu ya tofauti zetu za dini na uhusiano wa namna hii umekuwapo kwa muda mrefu, hivyo hatutarajii kuuvunja.**

Tumekuwa pia na mifumo ya kisiasa hasa tangu tulipoanza harakati za kupata uhuru. Vikaundwa vyama vya siasa kama silaha ya kuwafanya watu wawe pamoja ili kuwasilisha ajenda katika kutafuta uhuru wa nchi yetu. Vyama vilitusaidia kupata uhuru na baadaye tukaona tupanue wigo wa watu kujipambanua katika siasa. Tukakubali kuingia katika mfumo wa vyama vingi mwaka 1992 na mwaka 1995 tukafanya uchaguzi wa kwanza wa mfumo wa vyama vingi.

Tulikubaliana kwamba pamoja na kuwapo kwa mfumo ya vyama vingi vya siasa, haimaanishi kuwa kila Mtanzania ni mwanachama wa chama kimojawapo cha siasa, anaweza kuwa na mawazo tofauti na mwingine jambo ambalo ni kawaida kwa binadamu.

Hata hivyo, siku za karibuni zimeonekana chuki za waziwazi baina ya baadhi ya wanachama wa baadhi ya vyama vya siasa jambo ambalo kutokana na utamaduni wetu wa kuishi pamoja, linaleta sura mbaya ndani na nje ya nchi ambako tumekuwa mabalozi wazuri wa umoja na mshikamano.

Mafarakano ya kisiasa hayana afya kwa maendeleo ya nchi yetu. Nadhani wakati umefika sasa kujenga sifa njema ya taifa letu kama ambavyo tuna tofauti zingine za makabila na dini lakini tuko pamoja. Tunaweza kuwa na vyama vya siasa na tukasalia wamoja huku tukitambua kuwa Tanzania ni muhimu zaidi kuliko vyama vya siasa.

Kuendeleza migogoro ya kisiasa ni kulitenga kundi la wale wasiokuwa wanachama wa vyama vya siasa pamoja na kwamba siasa ndiyo huamua mustakabali wa maisha yao kwa maana ya elimu, uchumi na maendeleo kwa ujumla. Tuna kila sababu ya kuzika tofauti zetu ambazo zinaleta mivutano baina yetu na hatutaonekana wajinga kwa sababu tu tumeamua kuzungumza na kuanza upya kwa usawa na haki miongoni mwetu bila kundi lolote kukandamizwa na kuonewa.

Ni hivi karibuni, tumeshuhudia Rais Samia Suluhu Hassan akikutana na kiongozi wa chama kikuu cha upinzani na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu na kufanya mazungumzo kama viongozi lakini kama Watanzania, dada na kaka.

Pengine huu uwe mwanzo wa kufungua milango ya mazungumzo ndani ya nchi ili kufikia makubaliano kama watanzania wenye nia ya pamoja ya kujenga nchi. Suala la nani alianza kuomba kuonana na nani si la msingi sana na halitusaidii kama nchi. Muhimu ni mazungumzo na namna yatakavyotekelezeka kwa masilahi mapana ya nchi.

Hakuna ambacho kimewahi kushindikana katika mazungumzo ili mradi tu dhamira ya wazungumzaji iwe na nia njema kwa taifa na hapo ndipo kila mmoja atazungumza anachokiona na anachotamani kiwe kwa manufaa yetu sote na si kwa manufaa ya chama chake na jamaa zake.

Tunaweza kuondoa mtazamo wa kutumia vyama vya siasa kama njia ya kujipatia madaraka pekee bali vyama vya siasa vitumike kama njia ya kushindana kujenga nchi. Madaraka yanapita na nchi ipo. Vyama vya siasa kila siku vinazaliwa lakini nchi ni ileile na pia viongozi wanabadilika. Kwa hiyo tunakila sababu ya kukubaliana kuweka mifumo ya kujenga nchi kuliko kuvijenga vyama vyetu vya siasa kwa sababu siku moja vitapita pia kama ambavyo baadhi ya nchi baadhi ya vyama vimeshasahaulika ingali nchi zao ziko palepale.

Ushauri wangu ni kwamba kila mara tukumbuke sisi ni ndugu. Tukiweka tofauti zetu za kila aina pembeni tukabaki sisi, tunaweza kuutazama utu wetu kwa wengine yale ambayo tunapenda kutendewa, ndiyo tuyatende kwa wenzetu kwa sababu imeandikwa kipimo kilekile tupimiacho ndicho tutakachopimiwa. Hii pia ni kwa sababu mara zote huwa hatuyaoni makosa yetu kama tunavyoyaona makosa ya wengine. Muhimu zaidi, inapotokea hivyo basi dawa yake ni mazungumzo.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mwanamuziki akihama Sikinde, nyuma wanarekodi wimbo wake



Na Adam Fungamwango

ORCHESTRA Mlimani Park, wakati huo ikimilikiwa na Umoja wa Madereva Taxi nchini Tanzania, baadaye iliitwa DDC Mlimani Park ilipochukuliwa na Shirikia la Maendeleo la Dar es Salaam. Kwa sasa inaitwa Mlimani Park Orchestra. Hii ni baada ya wanamuziki kujitoa kwenye shirika hilo na kujitegemea.

Mtindo wake tangu ianzishwe mwaka 1978 ni 'Sikinde Ngoma ya Ukae'. Pamoja na kwamba ilianzishwa mwaka 1978 kutokana na asilimia 80 ya wanamuziki kutoka Dar International, ilitokea kuwa tishio kwa bendi zote ambazo zilizikuta.

Ikawa ndiyo mpinzani wa jadi wa bendi kongwe ya JUWATA Jazz Band, badala ya Urafiki Jazz. Sikinde ilishawahi kutwaa ubingwa wa muziki Tanzania katikati ya miaka ya 1980, kwenye mashindano ya muziki wa dansi Tanzania (MASHIBOTA). Hadi leo, bendi hiyo na Msondo Ngoma Music, ndizo zinazohesabiwa kuwa bendi kubwa zaidi na nembo ya muziki wa Tanzania.

Msondo yenyewe ilianzishwa mwaka 1964, ikiitwa NUTA Jazz, baadaye JUWATA Jazz, ikaja kuwa OTTU Jazz, ikitumia mtindo wa Msondo Ngoma. Mabadiliko ya majina hayo yalitokana na kubadilika pia kwa majina ya chama cha wafanyakazi ambacho awali kilikuwa Jumuiya ya Wafanyakazi (NUTA, JUWATA na baadaye OTTU). Mwisho ikaitwa Msondo Ngoma Music Band baada ya wanamuziki kuanza kujitegemea kutoka kumilikiwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) kwa sasa.

**Mabadiliko ya majina hayo yalitokana na kubadilika pia kwa majina ya chama cha wafanyakazi ambacho awali kilikuwa Jumuiya ya Wafanyakazi (NUTA, JUWATA na baadaye OTTU).**

Sikinde ni bendi iliyorekodi nyimbo nyingi ndani na nje ya nchi ambazo zilipendwa na zinaendelea kupendwa na vizazi vyote vitakavyokuja. Hata hivyo, kuna jambo ambalo baadhi ya mashabiki wa muziki hawalijui. Sikinde ni bendi ambayo ilirekodi nyimbo kadhaa ambazo zilitungwa na wanamuziki wake waliohama. Wao hawakuona taabu kurekodi wimbo wa mwanamuziki wake ambaye amehama.

Mara nyingi zamani mwanamuziki anaweza akawa ametunga na kuufanyia mazoezi wimbo fulani, halafu kwa bahati mbaya au nzuri akaihama bendi hiyo, wengi huondoka nao. Bendi ambayo ameondoka huwa haijishughulishi tena na wimbo huo badala yake mwanamuziki huyo anaupeleka kule alikohamia na kuurekodi. Hii imetokea mara nyingi na wiki ijayo nitaziorodhesha baadhi ya nyimbo za bendi kadhaa ambazo kabla zilikuwa kwenye bendi zingine.

Utashangaa kuwa wimbo wa bendi hii ambao unaufahamu ulitungwa na kuimbwa mpaka jukwaani na bendi nyingine, lakini mtunzi alihama, akaondoka na wimbo wake, kuupeleka bendi nyingine. Lakini Sikinde haikuwa hivyo. Wao ukiondoka, wanakwenda kurekodi.

Hii iliwasababishia mzozo na baadhi ya bendi na wanamuziki wake. Ndiyo maana kuna nyimbo kadhaa za Sikinde, ambazo pia zimerekodiwa na bendi zingine.

Tukianza na wimbo wa 'Nalala kwa Tabu'. Huu ulitungwa na Cosmas Thobias Chidumule, mwanzoni mwa miaka ya 1980. Kabla ya kuurekodi kwenye studio za Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD), alihama na kujiunga na Vijana Jazz Band.

Sikinde kwa kujua kuwa mtunzi wa wimbo huo amehama, hawakumwachia aende nao, walipokwenda kurekodi waliurekodi, ingawa kwa uungwana waliandika mtunzi ni Chidumule, ingawa hayupo.

Hapa sasa haikujulikana kama Vijana Jazz chini ya uongozi wa Hemed Maneti, hawakuona umuhimu na wao kuurekodi wimbo huo au Chidumule hakuupeleka.

Huenda ikawa hakuupeleka ili kuonyesha ana hazina ya nyimbo kwani ni kipindi hicho hicho akiwa bendi yake mpya ya Vijana Jazz, alichotunga na kurekodi nyimbo ambazo ni 'Nilitaka Iwe Siri', "Maisha Ni Safari Ndefu' na 'Unikubalie'.

Uongozi wa DDC Mlimani Park ulishtushwa na kushangazwa na uwezo mkubwa wa Chidumule kwani nyimbo hizo tatu alizotunga Vijana Jazz, zilitikisa nchi na kuiba mno bendi hiyo, huku wimbo aliouacha Sikinde nao ukionekana kupendwa mno na mashabiki. Ilibidi wapande nao na kumrudisha, licha ya kwamba aliondoka kwa 'figisu'.

Chidumule huyo huyo, katikati ya miaka ya 1980, alikwenda bendi ya Kurugenzi Jazz Band na kutunga wimbo wa 'Sinema ya Bure' lakini muda mfupi baadaye alirejea Sikinde na pia akaurekodi wimbo huo kwa jina la 'Majirani Huzima Redio'.

Kwa maana hiyo wimbo wa 'Majirani Huzima Redio' upo kwa Kurugenzi Jazz Band na kwa Sikinde, ingawa huu ni mwenyewe Chidumule aliamua kurekodi huku na huku kwa majina tofauti.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, Sikinde ilimpokea mwanamuziki Ramadhani Kinguti 'System'. Akawatungia wimbo unaitwa Wenye Nyumba Msiwaudhi Wapangaji. Kabla ya kurekodiwa, akahama. Kwa kawaida ilibidi ahame nao. Sikinde wao walikwenda kurekodi RTD, wakarekodi na wimbo huo, mtunzi akiwa ameshaondoka.

Hatua hiyo ilileta mzozo lakini mtunzi wa wimbo huo, Kinguti naye aliurekodi akiwa kwenye bendi aliyohamia ya Bicco Stars kwa jina la 'Wenye Nyumba'. Hadi leo nyimbo hizo ziko mbili, wa Sikinde na wa Bicco.

**Tuma semeji 0716 35 05 34**

# HADITHI

# Ajenda ya Siri-18

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

KATI ya watu wote waliotoa ushahidi, Eddy hakuona mwingine wa kuanza naye, isipokuwa mfamasia ambaye alikwenda kutoa ushahidi aliyemwuzia dawa ambazo zilikatisha uhai wa mfayabiashara huyo. Kazi ikazaa mapenzi. Eddy akayatumia pia mapenzi hayo kwenye kazi.

Ndiyo maana hadi wakati huo Mwahija akawa anamfahamu Eddy kwa jina la Danny, na anachojua ni mjomba wa Tina. Hata alipoombwa msaada wa kutafuta mahali ambapo mlinzi wa zamani wa nyumba hiyo wakati mauaji yanafanyika, Mwahija alifanya hivyo akijua anayemtafutia ni mjomba wa Tina.

Alilipata jina la mzee Kalango na mahali anapoishi Goba. Akamkabidhi Dan kwa anavyomjua yeye, ambaye pia kwa sasa ni mpenzi wake. Bila kujua huyo ni mpelelezi mashuhuri nchini na Afrika kwa ujumla, Eddy Kamal.

****************************

"Mwamba tayari nilishakata rufani zamani, kabla ya siku 30. Tangu siku ile uliponiambia una nia ya kutaka kuchunguza kama binti huyu mdogo ndiye aliyefanya jambo hili mwenyewe peke yake, au kuna mkono wa mtu nyuma yake."

"Vizuri sana bwana Tinga, du, kweli kila mtu na kazi yake. Mimi nilijua nikishamaliza kupeleleza, basi tunaweza kukata rufani."

Kilifuatia kicheko kutoka kwa Tinga kisha akamalizia "Wewe unajua kupeleleza tu, mambo ya sheria tuachie sisi. Hivi ulidhani ingewezekana, thubutu. Zikiisha siku 30 biashara imekwisha. Ungekuwa umefanya kazi bure ndugu yangu."

"Kumbe eee, nashukuru sana rafiki yangu."

"Sikia Eddy, hili ni suala ambalo wewe ulilianzisha. Na kwa sababu ni rafiki yangu, sikuona sababu ya kuacha kukuunga mkono. Ndiyo maana mimi sikutaka kukwambia jambo hili. Nilijua wewe uko mahiri kwenye upelelezi, nikakuacha ufanye kazi yako na mimi nikusaidie nikate rufani, halafu mengine tutajua baadaye," Tinga alimwagika.

"Okay, hiki ndicho kielelezo cha mwisho, kimetoka kwenye hoteli ya Moonlight, Sinza," alisema huku akimkabidhi.

"Ndugu yangu we kiboko, yaani hukuacha kitu."




**Itaanza kupitiwa tangu mwanzo upande wa mashtaka hadi mwisho upande wa utetezi ambao mwanzo msichana hakuwa na wakili wala vielelezo vyovyote tutakapoweka ushahidi wetu na hapo sasa tutaona kama kuna watu wengine nyuma ya hili.**

"Kwa jinsi nilivyomwona yule binti siku ile akilia, siwezi kuacha kitu."

"Sawa Eddy, nakuhakikishia mimi nitaisimamia kesi hii bure kama wakili upande wa utetezi kwa kutumia vielelezo vyote hivi ili tuone kama tunaweza kufanya kitu hapa.

Kesi itakuwa inasikilizwa kwenye Mahakama ya Rufani."

"Sawa tutakuwa wote. Ni lini tutarajie?"

"Wiki ijayo kwa taarifa nilizoletewa leo, kesi itaanza tena kunguruma. Itaanza kupitiwa tangu mwanzo upande wa mashtaka hadi mwisho upande wa utetezi ambao mwanzo msichana hakuwa na wakili wala vielelezo vyovyote tutakapoweka ushahidi wetu na hapo sasa tutaona kama kuna watu wengine nyuma ya hili.

Ngoja nikapitie kwanza leo usiku, nadhani wewe umeshajua kipi umekifanya," Tinga alisema akiwa ndani ya ofisi yake.

Eddy alitoka nje ya ofisi za Wakili Tenga na kwenda moja kwa moja hadi Tegeta kwa mpenzi wake Mwahija.

Alitokea kupendwa na familia ya Mwahija. Si kutokana na kwamba alikuwa anajali matatizo ambayo yanaweza kutatuliwa kwa urahisi akafanya hivyo bali pia alikuwa mcheshi, mnyenyekevu, adabu na heshima.

Kila anapofika anakuwa kivutio kwa mama yake mdogo Mwanabakari na mashemeji zake wa kike na wa kiume.

"Karibu mwanangu."

"Ahsante mama." Aliingia na kuketi kwenye kochi sebuleni.

Tayari alishakuwa mwenyeji kwenye nyumba hiyo.

Upesi mama aliingia chumbani na kuchukua simu yake akampigia Mwahija.

Ukweli ni kwamba Eddy alikwenda moja kwa moja na hakumwarifu mpenzi wake lakini alijua kuwa siku hiyo hakwenda kazini kwa sababu waliwasiliana asubuhi na akaambiwa hivyo.

Kwa sauti ya chini kama anayenong'ona, akamwambia:"We Mwahija uko wapi wee usituletee balaa we mtoto."

"Kwani vipi mama?"

"Mwenzio keshafika huku, uko wapi we mwana?"

"Nipo kwa shoga yangu Zubeda."

"Haya haya, fanya upesi, rudi."

Alikata simu. Sekunde chache baadaye, alitoka chumbani na kukaa na mgeni.

"Enhee baba, habari za kazi."

"Nzuri tu mama, sijui nyie huku."

"Hatujambo hivyo hivyo, mwenzio mguu huu unanipa tabu," Mwanabakari alisema huku akionyesha mguu wa kushoto.

"Tatizo ni nini mama?"

"Hata najua? Umeshtuka tu una wiki sasa."

"Okay, basi mama haitokuwa vizuri usijue tatizo ni nini wakati unauma, ni lazima ukacheki hospitalini ili kujua tatizo."

"Pesa yenyewe ipo baba? Hivi hapa mwenzio Mwahija, ndiyo huwa ananiletea dawa za kutuliza maumivu. Kuna za kunywa na kuchua, basi maisha yanaendelea, ndiyo najiona nina afadhali hata ya kutembea, japo kwa kuchechemea."

"Sawa mama, lakini huwezi kujua tatizo ndani likoje. Ngoja nitampigia daktari wangu, aje hapa kesho akuchukue na kukupeleka hospitalini akakufanyie vipimo kamili ili tujue tatizo hasa ni nini na baada ya hapo ndipo matibabu halisi yaanze."

Mama mdogo wa Mwahija, Mwanabakari, ni kama hakusikia au hakuamini alichosikia. Alitaka kumwambia arudie tena, lakini sauti haikutoka. Ghafla Mwahija aliingia.

"Nitashukuru sana baba, Mungu akubariki baba yangu, upate kikubwa zaidi ya hiki baba," Mwanabakari alishukuru huku akisimama na taratibu akaanza hatua za kutoka nje. Alifanya hivyo kwa makusudi ili kuwapisha Eddy na Mwahija. Kitendo cha yeye kuendelea kung'ang'ania hapo kusingewapa uhuru wa kutosha kujiachia.

"Amina mama," aliitikia Eddy.

Mwahija alikwenda kukaa ubavuni mwa Eddy.

"Mmh, mtu na mama yake, mmedanganyana nini?"

"Mama kaniambia eti tangu asubuhi ulivyoondoka hujarudi."

"Ndiyo ukajibu Amina mama?"

"Sasa unafikiri mimi ningejibu vipi?"

"Unanifunga kamba wewe."

"Ulikuwa wapi kwanza?"

"Hilo ndiyo ulilotaka kusema, ulikuwa unajibaraguza tu hapa."

"Ndiyo jibu hilo."

"Nilikuwa na shoga yangu Zubeda hapo nyumba ya nne ya tano kutoka hapa. Nilipeleka pesa ya upatu, basi maongezi yakazidi ndiyo mpaka muda huu." Mwahija alijibu akiwa anachezea kola na vifungo vya shati la mpenzi wake."

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# 'WATU WATANIELEWA TU'

## JANE MISSO AWAKABILI WANAOMUULIZA KUHUSU OMOYO



UKITAZAMA chati za muziki kwa sasa hapa Afrika Mashariki utakutana na wimbo, Omoyo Remix, kutoka kwa mwimbaji mkongwe wa Injili nchini, Jane Misso akishirikiana na Harmonize.

Tayari Harmonize ametangaza kuwa licha ya kuwekeza pesa nyingi katika utengenezaji wa muziki na video ya wimbo huo, hatachukua chochote kwenye mapato yake ili kumuunga mkono Misso na wanawake wote wanaomtumikia Mungu.

BT limekutana na Jane Misso jijini Dar es Salaam na kufanya naye mahojiano yafuatayo kuhusu kazi yake hiyo ambayo ameifanya na msanii wa Bongo Fleva, Harmonize.

**BT:** Sababu zipi zilifanya uwe kimya kwa muda mrefu?

**Jane Misso:** Nilikuwa kimya kwa sababu nilikuwa najiandaa. Kama unavyojua muziki wetu sio kama muziki mwingine ni lazima ukae utulie upate ujumbe wa kutoa kwa watu.

**BT:** Unadhani kwanini wimbo Omoyo umeendelea kufanya vizuri tangu ulipoutoa miaka 10 iliyopita?

**Jane Misso:** Kwakweli ni neema tu ya Mungu, ni wimbo ambao unazungumza na mioyo ya watu, unaonekana una ujumbe mzito sana ingawa kuna watu walikuwa hawaelewi sababu niliimba kilugha ila nadhani wamefafanuliwa na hii Remix.

**BT:** Kolabo yako na Harmonize imefanya nini kwenye maisha yako ya muziki?

**Jane Misso:** Kiukweli imenirudisha kwenye ramani pia imefanya nione kwamba nathaminika, ninapendwa sikutegemea kabisa kama kuna watu wananiwazia mema, nilijua nimemaliza kufanya kazi yangu na watu wanaburudika kwenye vilabu, kwenye mabaa, makanisani kumbe kuna watu wananitazama kwa namna tofauti, imenitia moyo na nimekuja na mtazamo mpya kabisa wa kufanya kazi kwa bidii.

**BT:** Kwanini ilikuwa rahisi kukubali kufanya kazi na Harmonize?

**Jane Misso:** Ilikuwa rahisi kwa sababu alikuja moja kwa moja kwangu akiwa na malengo yake na nia ya kutaka kufanya huu wimbo. Akasema wimbo Omoyo anaupenda sana na kuupenda tu haitoshi hivyo anaomba auenzi wimbo huu kwenye miaka zaidi ya 10 ili awe sehemu yake, niliona ni surprise kubwa, nilimuelewa vizuri sana.


**BT:** Kushirikiana na msanii wa Bongo Fleva hakujakuletea shida kwenye imani yako?

**Jane Misso:** Haijaniletea shida sema tu watu hawakutegemea ila nataka niwaambie hiyo ndio kazi iliyomleta Yesu duniani, kuwasogeza karibu watu walio mbali na Mungu kwahiyo mimi kufanya kazi na Harmonize ni kumwonyesha kuwa Mungu anampenda na Harmonize ni mtoto wa Mungu, watu wengi wameupokea vizuri wimbo nashukuru.

**BT:** Mipango yako ni ipi baada ya kuachia Omoyo Remix?

**Jane Misso:** Kwenye hii projekti na Harmonize kuna mipango mingi sana huko mbeleni, kabla ya hii nilikuwa nimeandaa nyimbo nyingi zenye ujumbe mzito ambazo zitakuja hapo baadaye.

# Ali Kiba anaweza kufilisiwa?



KAMA mahakama ya nchini Kenya itamtia hatiani Ali Kiba na kisha kuivunja ndoa yake na Amina Khalef, basi msanii huyo anaweza kufilisika kutokana na masharti ya hukumu atakayopewa kuyatekeleza.

Ni wazi Ali na Mkewe Amina, hawawezi tena kukaa pamoja kutafuta suluhu, kwa maana hiyo mwanamuziki huyo anatakiwa ndani ya siku 15, kujibu madai hayo ili mahakama hiyo iendelee na majuku yake.

Awali, inadaiwa mwanamuziki huyo ameshindwa kuheshimu wito na kujibu kesi iliyowasilishwa na mkewe.

Kiba alifunga ndoa na Amina mnamo Aprili 19, 2018, huko Mombasa.

Baadhi ya sababu ambazo mkewe anadai kushindwa kuendelea na ndoa yake ni, vitendo vya ukafiri, matusi na kukatishwa tamaa kutoka kwa wakwe zake na yeye mwenyewe.

Madai hayo ya talaka yamefunguliwa Februari 10, katika Mahakama ya Kadhi ya Mombasa, hivyo ilimpa Kiba siku 15, kujibu madai hayo.

Kwa mujibu wa nyaraka ya mahakama iliyoonekana na Star, Januari 8 mwaka jana, Amina alikwenda Mahakama ya Kadhi akitaka kukatisha ndoa yake na Kiba.

Amina anataka ndoa hiyo ivunjwe na anadai malipo ya Shilingi za Kenya 200,000 sawa na Shilingi milioni nne za Tanzania kila mwezi kwa ajili matunzo ya watoto na kulipia bima ya matibabu kwa watoto hao wawili.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HAALAND AIKATAA LIGI KUU ENGLAND

Majaliwa yake ni kutaka kucheza Hispania, hatapokea ofa kutoka timu yoyote ya EPL...

**DORTMUND, UJERUMANI**

ERLING Haaland ameamua kwamba, mustakabali wake utakuwa nchini Hispania, huku ripoti zikisema amezionya timu zinazomuwania kutoka Ligi Kuu ya England, kuwa hatasikiliza ofa zao msimu unaokuja wa joto.

Mshambulizi huyo Borussia Dortmund ndiye mchezaji anayesakwa zaidi duniani kwa sasa.

Katika Ligi Kuu ya England, EPL, Manchester City, Manchester United, Chelsea na Liverpool zinavutiwa nae, huku Bayern Munich na Paris Saint-Germain zote zikiwa na nia ya kumbakisha barani Ulaya.

Lakini kwa mujibu wa gazeti la Sport, Haaland anavutiwa tu na kuhamia Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, ambapo Barcelona na Real Madrid wanapigania saini yake.

Hayo mengi yaliwekwa wazi kwa City haswa wakati wa mkutano wa hivi majuzi kati ya viongozi wa Ligi Kuu na msafara wa Haaland.

Baba yake, Alf-Inge, aliwahi kuichezea man City na ilisemekana kuwa anamsukuma mwanawe kuelekea Etihad, lakini Haaland mdogo anataka kwenda LaLiga.

Sasa inaonekana kama mbio za farasi wawili kwa mustakabali wa Haaland, huku Real na Barcelona zote zikipanga kutupa kiasi kikubwa cha fedha kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway katika jaribio la kushinda mbio za kuwania saini yake.

Barcelona wamesalia na nia ya kumsajili Haaland na wanatumaini kumpa vitu ambavyo Real Madrid hawawezi.

Barcelona wako tayari kulipa kipengele chake cha kuachiliwa cha euro milioni 75 na wanataka kumpa mkataba wa miaka mitano wenye thamani ya jumla euro milioni 100, na pia wanafanya kazi ya kumshawishi Alf-Inge na wakala Mino Raiola kukubali ada yake kwa awamu.

Hilo linaweza kuwapa faida zaidi Real, ambao wanatamani sana kumsajili Haaland lakini wangependelea kumpata mwaka 2023, wakati mkataba wa Karim Benzema pale Santiago Bernabeu utakapokamilika.

Real Madrid kwa sasa akili yao ipo zaidi kwa Kylian Mbappe ambaye anaweza kutua hapo kwa uhamisho huru mara mkataba wake utakapomaliza mwishoni mwa msimu huu.

## KWA UFUPI

### KANE KUAMUA
HARRY Kane mwenye umri wa miaka 28, atasubiri hadi mwisho wa msimu kabla ya kuamua mustakabali wake pale Tottenham Hotsput, huku nahodha huyo wa timu ya taifa ya England, kwa sasa hataki kujadili kuongezwa kwa mkataba wake. ***(Standard)***

### ARSENAL WAKASIRIKA
ARSENAL wamekasirishwa kufuatia kushindwa kumpata mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 22, huku kocha Mikel Arteta sasa akikabiliwa na kinyang'anyiro cha kusuluhisha kitendawili cha mshambuliaji wa klabu hiyo.***(Mirror)***

### MADRID OFA KWA HAALAND
REAL Madrid wamewasilisha ofa ya mwisho kwa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, ambayo inaweza kuwa pigo kwa matumaini ya Manchester United, Chelsea na Manchester City ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway.***(Sport via Sun)***

### AZPILICUETA KUBAKIZWA
THOMAS Tuchel amesema, Cesar Azpilicueta bado ni "muhimu sana" kwa mipango yake ya Chelsea licha ya mkataba wa beki huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 32 kufikia ukingoni.***(Mail)***

### CESAR NA BARCA
BARCELONA wamempa Cesar Azpilicueta mkataba wa miaka miwili na chaguo la kurefusha kwa msimu zaidi huku wakipania kumnasa nyota huyo wa Chelsea kutoka Stamford Bridge.***(Fabrizio Romano via Express)***

### GAVI AWINDWA
CHELSEA ni miongoni mwa klabu zinazomuwinda kiungo wa kati wa Barcelona na Hispania, Gavi mwenye umri wa miaka 17. ***(El Nacional)***.

### EZE ANA FURAHA CRYSTAL
NYOTA Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 23 ana furaha katika klabu ya Crystal Palace huku kukiwa na ofa kutoka Newcastle United. ***(Standard)***

### KOUNDE AITAKA CHELSEA
MLINZI wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 23, anapendelea kuhamia Chelsea ikiwa ataondoka katika klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga. ***(Fichajes)***

### ZAHA KUONDOKA
WINFRIED Zaha mwenye umri wa miaka 29 raia wa Ivory Coast anaweza kuondoka Crystal Palace kipindi cha majira ya joto.***(Mail)***

### DE BEEK KUBAKIA EVERTON
KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 24, atajaribu kuachana jumla na Manchester United ili apate uhamisho wa kudumu kwa Everton msimu unaokuja wa majira ya joto.***(Mirror)***

### BERGWIJN AWANIWA MILAN
WINGA wa Tottenham Hotspur na Uholanzi, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 24 anaivutia AC Milan. ***(Calciomercato)***

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
LEEDS
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 3.61
X | 3.71
2 | 1.95

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GREALISH MAMBO MAGUMU MAN CITY



**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City walivunja benki ili kumsajili Jack Grealish lakini nyota huyo aliyetua hapo kwa fedha nyingi bado hajaweza kufikia matarajio.

Kiungo huyo alikosa mchezo wa jana Jumamosi dhidi ya Tottenham Hotspur kutokana na jeraha, lakini ameshindwa kutamba mara kwa mara kwenye kikosi cha kocha Pep Guardiola hata akiwa fiti.

Lakini kwa nini imekuwa hivyo na je, mchezaji huyo anayevaa jezi namba 10 anawezaje hatimaye kupata nafasi kwa vinara hao wa Ligi Kuu England?

Grealish mwenye umri wa miaka 26, alikua mchezaji ghali zaidi wa Uingereza wa wakati wote alipojiunga na City kutoka Aston Villa kwa pauni milioni 100, Agosti.

Hata wakati wa kusaini kwa klabu yenye utajiri mkubwa City, aina hiyo ya bei huja na shinikizo fulani la kutoa - na haraka.

Lakini hadi sasa, Grealish hajakaribia kuwa kwenye kiwango bora kilichomfanya aonekana hadi kusajiliwa kwa fedha ndefu.

Alikuwa na kiwango bora kule Villa na alimaliza msimu uliopita akiwa mmoja wa wachezaji watano wa EPL walioweka rekodi ya kutoa pasi za mabao.

Msimu huu amefunga mabao mawili pekee ya ligi na wastani huo umeshuka hadi asilimia 0.14 kwa 90.

# Allegri afurahia sare ya Juve kwa Torino

**TURIN, Italia**

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri amesisitiza kwamba sare ya 1-1 na Torino kwenye Uwanja wa Allianz siku ya Ijumaa iliendeleza "msururu mzuri" wa timu yake.

Wenyeji walichukua nafasi ya uongozi kwa bao la Matthijs de Ligt aliyefunga kwa kichwa kipindi cha kwanza, lakini Andrea Belotti alisawazisha na Juve wakajitahidi kutengeneza nafasi za maana katika kujibu, na kushindwa kulenga goli katika kipindi cha pili.

Kibibi kizee hicho cha Turin sasa kimesalia kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa Serie A, pointi nane nyuma ya viongozi AC Milan ambao wamecheza mchezo mmoja zaidi, na pointi tatu tu mbele ya Atlanta katika nafasi ya tano, ambao wana michezo miwili mkononi.

Akizungumza na DAZN baada ya mchezo huo, Allegri alionekana kuridhishwa na matokeo hayo na kiwango cha timu yake.

"Ni muhimu kwa sababu, kwa uhakika, tulifuatilia matokeo chanya ambayo tumekuwa nayo katika miezi miwili hadi mitatu iliyopita," alisema.

"Haikuwa rahisi, hatukuwa na kasi sana ikilinganishwa na Torino, lakini tulicheza mchezo mzuri.

"Kwa kushangaza, tuliruhusu bao katika dakika zetu bora zaidi. Katika kipindi cha kwanza tulikuwa na hali mbili au tatu ambazo tungeweza kufunga, lakini sio kipindi cha pili.

"Kipindi cha pili hatukuwa bora sana, lakini nadhani ni njia ya kawaida, ni jambo la kawaida unapocheza kwenye ligi, haswa unapolenga kuingia kwenye nne bora, kwa hivyo sare sio, tumeridhika nayo."



## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI
CHEZA
SHINDA

# BARAZA AKANUSHA KUITOSA KAGERA SUGAR

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza amekanusha taarifa ya kuhusishwa kupata ofa ya kukinoa kikosi cha timu ya Taifa ya Vijana chini ya umri wa miaka 20.

Hivi karibuni kulikuwa na taarifa kwa kocha huyo kuhusishwa kufanya mazungumzo na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, TFF, kwa ajili ya kupewa jukumu la kukinoa kikosi hicho cha vijana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema hizo ni tetesi na hakuna ukweli juu ya taarifa hizo kwa sababu bado ana mkataba wa kuitumikia Kagera Sugar.

Alisema akili na nguvu zake amezielekeza katika timu yake kuhakikisha inapata matokeo mazuri katika michezo yao iliyobakia ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Hizo ni taarifa za mitandao, hakuna ukweli wowote kuhusu mazungumzo na TFF kunitaka kuwa kocha wa timu ya taifa ya vijana chini ya umri wa miaka 20, bado niko Kagera Sugar kuhakikisha nasaidia timu yangu kupata matokeo mazuri katika mechi zilizobakia," alisema.

"Msimu uliopita hatukuwa katika nafasi nzuri na tulicheza mechi za mwisho kwa presha jambo hilo hatutaki lirudiwe msimu huu na kwa sasa akili na nguvu zetu zipo kwenye kupata matokeo mazuri kwenye mechi zijazo za ligi."



Baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wakijiandikisha kwa ajili ya kuchukua namba kwa ajili ya mashindano ya Kilimanjaro Marathon yanayotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha Mlandege akunwa na ushindi

**Hawa Abdallah, Zanzibar**

KOCHA msaidizi wa Mlandege, Jaala Abdallah amesema licha ya udhaifu walionao katika timu hiyo, lakini wachezaji wake walicheza vizuri na kupata ushindi wa 2-1 dhidi ya Uhamiaji FC kwenye Ligi Kuu Zanzibar.

Ushindi huo umeifanya Mlandege kupanda kwa nafasi moja kutoka ya nane hadi saba na kuishika Uhamiaji kwa nafasi moja.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo juzi, Abdallah alisema mchezo ulikuwa mgumu kwa dakika zote na wachezaji hawakuonesha kuchoka kwa kuwa walijua lengo ni kuhakikisha wanapata alama tatu zitakazowafanya wasonge mbele katika mzunguko huu wa 19.

"Tulicheza vizuri, kipindi cha kwanza wachezaji walijituma na wenzetu wa upinzani walionesha wako fiti, na kipindi cha pili Uhamiaji waliamka na mashambulizi yalifanywa kwa zamu lakini bahati ilikuwa kwetu," alisema.

Hata hivyo, aliongeza kusema hivi sasa wanajipanga kueleke mchezo unaofuata wa mzunguko wa 20 dhidi ya Maafande wa KVZ ambao utapigwa Februari 26 katika dimba la Amaan.

Ligi hiyo inaendelea na mzunguko wake wa 19 ambapo leo Taifa Jang'ombe itacheza na Malindi, wakati KVZ wataikaribisha Selem View michezo yote ikipigwa dimba la Amaan.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 20/02/2022


| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4678 | Fiorentina vs Atalanta | 2.59 | 3.48 | 2.59 |
| 15:00 | 1936 | Dundee Utd vs Rangers | 8.88 | 5.13 | 1.30 |
| 15:00 | 4195 | Nice vs Angers | 1.71 | 3.69 | 4.79 |
| 16:00 | 1560 | Lamia vs Apollon Smyrnis | 1.97 | 3.12 | 4.06 |
| 16:00 | 2999 | Alanyaspor vs Trabzonspor | 2.96 | 3.30 | 2.31 |
| 16:00 | 3199 | Espanyol vs Sevilla FC | 3.35 | 3.25 | 2.21 |
| 16:00 | 4863 | Fatih Karagumruk vs Sivasspor | 2.52 | 3.22 | 2.72 |
| 16:00 | 5524 | Midtjylland vs Aalborg | 1.70 | 3.65 | 4.73 |
| 16:15 | 2108 | FC Sion vs FC Zurich | 3.30 | 3.50 | 2.06 |
| 16:30 | 1981 | Austria Klagenfurt vs SCR Altach | 1.81 | 3.56 | 3.75 |
| 16:30 | 2057 | RB Salzburg vs Wolfsberger AC | 1.26 | 5.40 | 8.10 |
| 16:30 | 3099 | Twente vs GO Ahead Eagles | 1.71 | 3.64 | 4.53 |
| 16:30 | 4883 | Feyenoord vs Cambuur | 1.12 | 8.23 | 15.68 |
| 17:00 | 2630 | Venezia vs Genoa | 2.50 | 3.25 | 2.85 |
| 17:00 | 4818 | St Etienne vs Strasbourg | 2.93 | 3.33 | 2.36 |
| 17:00 | 5458 | Rennes vs Troyes | 1.36 | 4.88 | 8.17 |
| 17:00 | 5505 | Lorient vs Montpellier | 2.34 | 3.24 | 3.04 |
| 17:00 | 5508 | Reims vs Brest | 2.35 | 3.23 | 3.03 |
| 17:00 | 5987 | Leeds vs Manchester Utd | 3.61 | 3.71 | 1.95 |
| 17:30 | 4870 | Bayern Munchen vs Greuther Furth | 1.06 | 12.00 | 26.00 |
| 18:00 | 2234 | Coquimbo vs CD Palestino | 2.80 | 3.13 | 2.36 |
| 18:00 | 2687 | Celtic vs Dundee FC | 1.11 | 8.30 | 19.76 |
| 18:00 | 5973 | Nordsjalland vs Brondby | 2.96 | 3.45 | 2.24 |
| 18:15 | 3579 | Valencia vs Barcelona | 3.40 | 3.45 | 2.10 |
| 18:15 | 3829 | Volos vs Olympiakos | 6.50 | 3.94 | 1.50 |
| 18:30 | 2231 | Servette Geneva vs FC Luzern | 1.95 | 3.54 | 3.59 |
| 18:30 | 3525 | Maritimo vs Famalicao | 2.46 | 3.20 | 2.81 |
| 18:30 | 3563 | Grasshoppers vs BSC Young Boys | 4.04 | 3.70 | 1.79 |
| 18:45 | 3337 | PSV Eindhoven vs Heerenveen | 1.15 | 7.10 | 13.81 |
| 18:45 | 4431 | Utrecht vs Vitesse Arnhem | 1.80 | 3.62 | 4.02 |
| 19:00 | 2506 | Fenerbahce vs Hatayspor | 1.72 | 3.74 | 4.42 |
| 19:00 | 4319 | Sturm Graz vs Rapid Vienna | 2.02 | 3.46 | 3.17 |
| 19:00 | 5851 | Senica vs SKF Sered | 2.94 | 3.27 | 2.20 |
| 19:05 | 4055 | Bordeaux vs Monaco | 4.67 | 4.08 | 1.65 |
| 19:30 | 1516 | Borussia Dortmund vs Monchengladbach | 1.59 | 4.48 | 4.68 |
| 19:30 | 3169 | Wolverhampton vs Leicester | 2.27 | 3.20 | 3.25 |
| 20:00 | 3302 | Inter vs Sassuolo | 1.30 | 5.99 | 8.18 |
| 20:00 | 4243 | Bnei Sakhnin vs Nazareth Ilit | 1.98 | 3.23 | 3.52 |
| 20:00 | 4906 | Copenhagen vs Odense | 1.45 | 4.33 | 6.50 |
| 20:30 | 2532 | Aris Salonica vs PAOK | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 20:30 | 3453 | Betis vs Mallorca | 1.58 | 4.11 | 5.41 |
| 20:30 | 4877 | AEK Athens vs PAS Giannina | 1.62 | 3.70 | 5.33 |
| 21:00 | 1660 | Sporting Lisbon vs GD Estoril | 1.25 | 5.54 | 10.88 |
| 21:15 | 2834 | Maccabi Tel Aviv vs Hapoel Haifa | 1.19 | 5.80 | 11.60 |
| 21:30 | 3058 | Hertha BSC vs RB Leipzig | 5.58 | 4.28 | 1.53 |
| 22:30 | 1517 | CD Trofense vs Mafra | 2.77 | 3.21 | 2.42 |
| 22:45 | 3153 | Marseille vs Clermont Foot | 1.47 | 4.38 | 6.37 |
| 22:45 | 4997 | Udinese vs Lazio | 3.09 | 3.34 | 2.29 |
| 23:00 | 5728 | Moreirense vs Porto | 8.84 | 5.10 | 1.31 |
| 23:45 | 2030 | Tondela vs Sporting Braga | 5.14 | 3.96 | 1.59 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Februari 20, 2022

Nipashe

**Haaland aikataa Ligi Kuu England** HABARI UK 21



Wachezaji wa Yanga, Abdalah Shaibu 'Ninja', Denis Nkane na Kibwana Shomari wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania bara dhidi ya Mtibwa Sugar utakaopigwa Jumatano kwenye dimba la Manungu Turiani, Morogoro.
**PICHA: Yanga**

# SIMBA KAZI KAZI NIGER

## Inashuka leo kuwakabili US Gendamarie waliochezea kichapo cha mabao 5, halafu itapaa zake juu kwa juu Morocco...

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI pekee kwenye michuano ya kimataifa, timu ya Simba, leo watakuwa ugenini kwenye mji wa Niamey nchini Niger kucheza mechi ya pili ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika hatua ya makundi, dhidi ya US Gendamarie.

Simba ambayo ilisafiri Alhamisi jioni ikiwa na wachezaji 23, benchi la ufundi na baadhi ya viongozi, itacheza mechi yake hiyo kwenye Uwanja wa General Seyni Kountche nchini humo, ikisaka ushindi, au angalau sare ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kutinga hatua ya robo fainali kutoka kundi lake D.

Jumapili iliyopita, Simba ilipata ushindi mnono wa mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Asec Mimosas, hivyo na sasa inashika nafasi ya pili na ushindi unaweza kuifanya kuwa kileleni mwa msimamo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu ya Simba, Ahmed Ally amesema kuwa kila kitu kimekwenda vizuri na kilichobaki ni kuingia uwanjani na wachezaji kufanya kile ambacho wanachama, mashabiki wa Simba na Watanzania kwa ujumla imewatuma.

"Wanasimba watarajie makubwa, wasiwe na hofu hata kidogo, Simba ilikofikia kwa sasa haiogopi nchi, haiogopi kiwanja, wala haiogopi mpinzani. Simba imeshinda Zambia, imeshinda DRC Congo, imeshinda Botswana, imeshinda Swaziland, popote pale ambapo mpinzani amekaa vibaya, basi tutashinda," alisema Ally.

Aliongeza; "Tumeshaachana na ule mpira wa kushinda nyumbani peke yake, kwa sasa lengo letu kubwa ni kushinda popote pale na tumeshafanya hivyo."

Alisema lengo la kwanza kwa timu hiyo ni kutopoteza hata mechi moja kati ya mbili ambazo itacheza na lengo la pili ni kushinda mechi zote mbili.

Wawakilishi hao wa Tanzania wanapambana na timu ambayo imetoka kupoteza mechi ya kwanza ugenini dhidi ya RS Berkane ya Morocco, ambapo ilichapwa mabao 5-3.

"Timu hii imepoteza mechi yake ya kwanza, hivyo tunajua haitokubali kupoteza mechi ya pili kirahisi, lakini pia sisi hatutokubali kupoteza kirahisi mechi ikiwa nyumbani, hayo yote tunayajua, ndiyo maana tunakwenda huko tukijua mechi ni ngumu, lakini tutapambana kuhakikisha tunaipigania na kuipa heshima bendera ya Simba na Tanzania kwa ujumla," alisema.

Hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa historia ya Tanzania na klabu ya Simba kucheza na timu kutoka Niger.

Si timu ya taifa, Taifa Stars au klabu yoyote nchini ambayo imeshawahi kucheza na timu kutoka nchini humo.

Simba itawakosa wachezaji watano kwenye mechi hiyo kutokana na sababu za majeruhi na matatizo ya kifamilia.

Wachezaji hao ni Chris Mugalu, Hassan Dilunga na Kibu Denis ambao ni majeruhi, huku Mzamiru Yassin na Rally Bwalya wakiachwa kutokana na matatizo ya kifamilia.

Ahmed alisema kuwa baada ya mechi hiyo, kikosi hicho ambacho kitakuwa nje ya nchi kwa siku 10, kinatarajia kukaa nchini Niger kwa siku nne, kabla ya kupaa kwenye Morocco, Februari 25 ambapo itacheza na RS Berkane, tarehe 27, na kitatua nchini tarehe 28 kukabiliana na Biashara United kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Machi 3 mwaka huu.

# Nabi hataki mchezo Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amewataka wachezaji wake kuzingatia mazoezi ili kuhakikisha wanapata pointi tatu dhidi ya Mtibwa Sugar, kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga watakuwa ugenini mbele ya wakata miwa hao wa Manungu katika mchezo huo utakaopigwa Jumatano katika uwanja huo wa Manungu, Turiani Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nabi alisema wamefanya mazoezi ya kutosha kwa aina ya uwanja ambao wanaenda kucheza, kazi kubwa iliyopo kwa wachezaji wake ni kuzingatia maelekezo aliyowapa na kuhakikisha wanapata pointi tatu katika mchezo huo.

Alisema ana imani kubwa wachezaji wake wakizingatia maelekezo na kufanyia kazi majukumu aliyowapa kulingana na ubora na madhaifu ya wapinzani wake ana imani ya kupata matokeo mazuri dhidi ya Mtibwa Sugar.

"Tunatambua hali halisi ya viwanja tunavyokwenda kucheza mechi za ugenini sio bora kama Benjamin Mkapa, uwanja isiwe sababu tukiwa hapa tukapoteza pointi mbili dhidi ya Mbeya City, lakini tulifanikiwa kupata pointi tatu ugenini na viwanja sio vizuri ," alisema Nabi.

"Wachezaji wanapaswa kuzingatia maelekezo ya mazoezi na kuhamishia katika mechi, haitakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wetu nao wako imara na wanahitaji pointi kama ilivyo kwetu," alisema Nabi.

Alisema amefanya maboresho katika kila sehemu huku akiimarisha zaidi safu yake ya ulinzi kwa sababu ya kukosa baadhi ya wachezaji akiwemo Dickson Job ambaye anatumikia adhabu ya kufungiwa mechi za ligi hiyo pamoja na kombe la Shirikisho.

Job alifungiwa na Kamati ya saa 72 ya Bodi ya Ligi Tanzania na kutakiwa kulipa faini ya laki tano, kwa kosa kumkanyanga mchezaji wa Mbeya City, Richardson Ng'ondya.

9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042